

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kwanza - Tarehe 10 Juni, 2003

(*Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi*)

DUA

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Wajumbe wafuatao waliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi zao Bungeni:-

Mhe. Salim Omar Ali
Mhe. Bakar Shamis Faki
Mhe. Khalifa Mohammed Issa
Mhe. Mwadini Abass Jecha
Mhe. Shoka Khamis Juma
Mhe. Ali Said Juma
Mhe. Nazir Mustafa Karamagi
Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa
Mhe. Mohamed Juma Khatib
Mhe. Abu Towagale Kiwanga
Mhe. Mchande Salim Mchande
Mhe. Sumri Abdallah Salum Mohamed
Mhe. Edward Nzirye Ndeka
Mhe. Omar Juma Omar
Mhe. Karim Said Othman
Mhe. Mohamed Ali Said
Mhe. Khamis Ali Saleh
Mhe. Masoud Abdallah Salim
Mhe. Ali Said Salim

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kazi ya kuwaapisha Wabunge wapya imekwisha, lakini napenda kutambua kuwepo Bungeni kwa Mbunge wa zamani, aliyepoteza Ubunge wake kwa sababu ya kufukuzwa na Chama chake cha CUF akashinda kesi Mahakamani na sasa amerudishiwa Ubunge wake, Mheshimiwa Zamda Bozzen. (*Makofi*)

Vile vile Waheshimiwa Wabunge, napenda kutambua kuwepo kwa wageni kutoka Jamhuri ya Rwanda katika *Gallery* ya Bunge. Ni ujumbe wa Wabunge sita, ambao unaongozwa na Spika wa Bunge la Rwanda, Mheshimiwa Vincent Biluta.

Tunaendelea na *Order Paper*.

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ni taarifa ile ya kawaida kuhusu Miswada iliyopitishwa na Bunge hili katika Mkutano uliopita wa Aprili. Taarifa ni kwamba, Mkutano huo ulipitisha Miswada sita na yote imeshapata kibali cha Mheshimiwa Rais na sasa ni sheria za nchi Na. 7, 8, 9, 10, 11 na 12 za Mwaka 2003.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):

Nakala za matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha Mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali yanaanza saa tatu na nusu, kwa hiyo, tutakwenda mpaka saa nne na nusu kabla kipindi cha maswali hakijaisha. Mheshimiwa Dr. Kabourou, uliza swali lako.

Na. 1

Maafa yaliyotokana na mafuriko - Kigoma Mjini

MHE. DR. AMANI W. KABOUROU aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo mwezi Machi mwaka 2003 yalitokea mafuriko makubwa Kigoma Mjini ambayo yalisababisha maafa makubwa ya hali na mali na kuvunjika kwa zaidi ya nyumba hamsini kwenye maeneo ya Gungu, Buzebazeba, Kibirizi, Kikungu na kadhalika:-

- Je, Serikali kupitia Kamati yake ya Maafa inalifahamu tatizo hilo na imechukua hatua gani?
- Je, Kamati hiyo ilitoa msaada wowote kwa waathirika na ni msaada wa aina gani uliotolewa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Amani Walid Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya mvua kubwa iliyonesha Mjini Kigoma na kusababisha maafa. Hilo tunalifahamu. Kupitia Kamati ya Maafa, Serikali ilitathmini maafa yaliyotokea Kigoma Mjini tarehe 08 Machi, 2003 kufuatia mvua kubwa iliyonesha kuanzia saa 8.30 mchana hadi saa 11.30 jioni. Tathmini imeonyesha kuwa mvua hiyo ilisababisha uharibifu wa nyumba 265 kwa viwango mbalimbali. Aidha, jumla ya uharibifu wa mali ulikuwa shilingi 24,943,000/= na jumla ya watu 1,747 waliathirika pia kwa viwango tofauti.

(b) Mheshimiwa Spika, kufuatia tukio hilo, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ilituma mahema 42 ya kutumiwa na wananchi katika kuijandaa kupata makazi na Kamati ya Maafa ya Mkoa wa Kigoma, ilipokea na kutoa misaada mbalimbali kwa waathirika yenye jumla ya shilingi 27,035,000/=. Misaada hiyo ni kama ifuatavyo:-

- Unga wa mahindi kilo 1,400;
- Maharage kilo 1,635;
- Mahindi kilo 12,906;
- Njegere kilo 1,950;
- Mchele kilo 835;
- Mablanketi 100;
- Sabuni aina ya foma miche 100;

- *Plastic sheets* 70 zenyne ukubwa wa mita 4 x 5;
- *Plastic sheets rolls* 2 zenyne urefu wa mita 200;
- Madumu ya *plastic* 50 (yenye ujazo wa lita 20);
- Ndoo za *plastic* 50;
- Vitenge jozi 75; na
- Nguo aina ya mitumba *bale* moja.

Mheshimiwa Spika, misaada hiyo ilitokana na fedha zilizochangwa na Taasisi na Mashirika ya Misaada ya Kimataifa kama ifuatavyo:-

1. Halmashauri ya Mji Kigoma/Ujiji (Sh. 609,000/=);
2. *UNICEF* (Sh. 1,500,000/=);
3. *Tanzania Red Cross Society* (Sh. 750,000/=);
4. *World Food Programme* (Sh. 22,000,000/=);
5. *Neighbours Without Borders* (Sh. 176,000/=); na
6. *International Islamic Relief Organization* (Sh. 2,000,000=).

Mheshimiwa Spika, hali sasa ni shuwari na wananchi wanaendelea na shughuli za maendeleo ya kijamii kama kawaida.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swalii moja fupi la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa ni muda mrefu umepita tangu tumepokea taarifa kwamba, Serikali ina mpango wa kutengeneza sera maalum ambayo inasimamia suala la maafa, naomba kujua utaratibu huo umefikia wapi na kwa nini Serikali inachelewesha suala hilo kiasi kwamba suala la kushughulikia maafa linaendeshwa bila *policy* maalum?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, habari aliyoisema ni kweli na Serikali imeshawahi kusema hata hapa Bungeni kwamba, tupo katika maandalizi ya kutayarisha sera na kama anavyojua sera ni *document* muhimu katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Kwa hiyo, tunafikiri ni wajibu wa Serikali kushirikisha wadau wote muhimu ili sera hii itoke ikiwa imekamilika. Kwa hiyo, sio kweli kwamba, Serikali inafanya makusudi kuchelewesha, lakini maandalizi yake yanahitaji utaratibu ambaa umekamilika zaidi. Kwa hiyo, baada ya muda mfupi sera hiyo inaweza kukamilika.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nina swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa maafa yamekuwa yakirudia kwa aina ile ile kila wakati; na kwa kuwa mpaka sasa sera haijakuwa tarayi; je, Waziri atakubaliana nami kwamba kwa kukosa sera na kwa kuwa maafa yale yale yanarudia na kwa kuwa hatujapata ufumbuzi wa yale matatizo ya mafuriko au maafa ambayo tungeweza kuyakabili yanatokana na kukosa hii sera?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu aina mbalimbali za maafa kulingana na jiografia ya nchi, tumeshafanya utafiti na kujua aina fulani fulani za maafa ambayo yanaweza yakajitekeza katika kanda zetu za Tanzania. Kwa hiyo, tunayo *disaster map* ya nchi na nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata tungekuwa na sera, haiwezi kuzuia maafa haya, yatatokea tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yapo maafa ambayo yanababishwa na watu lakini yapo maafa ambayo hatuwezi kutarajia ambayo yanaweza yakatokea. Mmeona jinsi maafa kama hayo yanavyotokea, kwa mfano, mwaka 2002 mmeona kuna matetemeko ambayo ni ajali ambazo Mwenyezi Mungu, ametuwekeea. Kwa hiyo, hata kama tungekuwa na sera hatuwezi kuzuia baadhi ya maafa.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba, pamoja na kwamba hatuna sera, hivi sasa upo utaratibu wa kudumu na unaoeleweka na ngazi zote za Serikali za kushughulikia maafa mbalimbali. Tunazo Kamati za Maafa kutoka kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya, ambazo kazi na wajibu wake unajulikana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi kwani hivi sasa Serikali inao utaratibu na itaendelea na utaratibu huu hadi hapo sera itakapokuwa imekamilika.

Na. 2

Ujenzi wa Ukumbi Mpya wa Bunge

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2005 upo uwezekano wa Tume ya Uchaguzi kugawa baadhi ya Majimbo likiwemo Jimbo la Ukonga, jambo litakalosababisha ongezeko la Wabunge; na kwa kuwa kuna dalili pia kwamba idadi ya Wabunge wa Viti Maalum inaweza kuongezeka kutoka asilimia ishirini hadi asilimia thelathini; na kwa kuwa Ukumbi wa sasa wa Bunge ni mdogo kiasi kwamba hautaweza kumudu ongezeko hilo la Wabunge kwa mwaka huo:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya Ujenzi wa Ukumbi mpya na mkubwa wa Bunge kabla ya Novemba 2005?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba kutokana na Wabunge kukaa muda mrefu (saa saba kwa siku) kwenye viti vidogo na nafasi finyu ndani ya Ukumbi wa sasa huwa wanaumia na wanaathirika afya zao na hivyo ni hatari kwa maisha yao ya baadaye?
- (c) Je, Serikali haioni kwamba kutokana na kukaa muda mrefu sana kwa siku ikilinganishwa na Mabunge karibu yote duniani, Wabunge wa Tanzania wanastahili posho kubwa zaidi ya vikao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na kuapishwa mbele yako leo asubuhi hususan wale wa CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inajua kwamba, Ukumbi huu wa Bunge hautoshelezi mahitaji ya sasa na ya baadaye kikamilifu. Kwa sababu hiyo, Serikali imetenga fedha kuanzia Bunge hili, endapo Waheshimiwa Wabunge, mtapitisha kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuanza kujenga Ukumbi mpya wa kisasa na utakaokidhi mahitaji yote muhimu kwa shughuli za Bunge. Kazi ya ujenzi itaanza mara moja Waheshimiwa Wabunge mkipitisha hoja hiyo. Ukumbi huo utajengwa hapa Dodoma. Ni nia ya Serikali kuona ukumbi huo umekamilika ifikapo mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la posho ya vikao kwa Waheshimiwa Wabunge, lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge katika kifungu (c), naomba tusubiri kwani Tume ya Huduma za Bunge inalifanya kazi na Mwenyekiti wetu ambaye ni Mheshimiwa Spika, atalitolea taarifa rasmi, wakati muafaka utakapofika.

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa suala la posho nililihusisha na muda mrefu wanaokaa Wabunge wa Tanzania kulinganisha na Wabunge wengine, naomba Mheshimiwa Waziri alihuushe na yeze.

Pili, kwa kuwa waandishi wa habari ambaa wanafanya kazi nzuri sana ya kuripoti mambo yanayoendelea Bungeni na wenyewe wanakaa katika hali ngumu kwa kuandika kwenye mapaja yao badala ya mezani. Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi kuwaandalia mazingira mazuri ya meza za kuandikia ili wawewe kuripoti habari za Bunge kwa ufasha? (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):

Mheshimiwa Spika, nilifahamu *nature* ya swali lako la (c), juu ya posho ya vikao kutohakana na muda mrefu zaidi wanaokaa Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana nimesema jambo hili wanatafakari Tume, kwa sababu kwa mujibu wa utaratibu wetu masuala yanayohusu maslahi ya Waheshimiwa Wabunge yanashughulikiwa na Tume. Kwa hiyo, nilifahamu *nature* ya swali lako na ndiyo maana nikaiachia Tume ambayo kwa kweli inahusika na haya na mengine ambayo hukuyasema.

Lakini pili, ukumbi mpya utakaojengwa nimesema utakidhi shughuli zote za Kibunge, ikiwa ni pamoja na shughuli hizo za waandishi wa habari. Katika ukumbi mpya tutakuwa na sehemu maalum, kwenye michoro nafikiri Mheshimiwa Spika, wakati fulani aliiweka kule *Library* na tukaiona. Utakuta kuna eneo maalum la waandishi wa habari, tutakuwa na mahali pa kukaa waandishi wa habari wanaoandika na sehemu maalum ambapo kutakuwa na vinasa sauti hivi vya *TV* ambavyo vitakwenda kwa mujibu wa utaratibu wa sasa wa sayansi na teknolojia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, asiwe na wasiwasi hayo yote yamezingatiwa katika mchoro wa jengo jipya la Bunge.

Na. 3

**Umuhimu wa Utafiti Kwenye Sehemu
za Taaluma ya Juu****MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa utafiti ni gharama lakini ni moja kati ya shughuli muhimu sana kufanyika kwenye sehemu zote za taaluma ya juu na kwa wataalam wenyewe hasa katika Vyuo Vikuu; na kwa kuwa hadhi ya Chuo cha Elimu kwa wanafunzi husifika kwa kupata faida, aina na uzito wa tafiti zinazofanywa; na kwa kuwa utafiti pia unawasaidia Wahadhiri wa Vyuo mbalimbali vya elimu ya juu kuweza kupandishwa vyeo kutohakana na utafiti walioufanya:-

- (a) Je, Serikali inaweza kutueleza kwa nini kwa muda wa miaka miwili mfululizo haikutenga kwenye bajeti zake fedha kwa ajili ya utafiti kwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba hiyo ni njia mojawapo ya kushusha hadhi ya Chuo hicho, elimu kwa wanachuo na kuwakosesha wahadhiri nafasi ya kupanda vyeo kwa muda muafaka?
- (c) Je, Serikali sasa inaweza kutoa ahadi na kauli ya uhakika kwamba itaweka fedha za kutosha katika bajeti yake ya 2003/2004 kwa ajili ya utafiti kwa Chuo hicho?

NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mbunge wa Mikunguni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kama ilivyo kwa Vyuo Vikuu vingine vya umma ni kutoa mafunzo, ushauri na kufanya utafiti. Katika kutekeleza majukumu hayo, Chuo hupata ruzuku toka Serikalini kwa ajili ya kugharamia miradi, wanafunzi, mishahara ya watumishi na shughuli nyingine za uendeshaji. Gharama zingine hulipwa kutohakana na mapato ya Vyuo vyenye vyeo kutohakana na shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilipata fedha jumla ya shilingi za Kitanzania 4,089,377,159/= kwa ajili ya kufanya utafiti kati ya miaka 2001/2002 na 2002/2003, shilingi 30,000,000/= zikiwa zimetokana na vyanzo vyake vya mapato kwa ajili ya utafiti. Aidha, hali ya utafiti katika Chuo Kikuu cha Sokoine hajashuka kwa vile utafiti unaendelea kufanyika, tafiti 124 zimefanyika, matokeo ya tafiti hizo yapo na Wahadhiri wameendelea kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kadri uchumi wa nchi unavyokua na pato la Serikali kuongezeka, fedha zaidi zitatengwa. Hata hivyo, kwa kuwa Chuo hupewa *ceiling*, jukumu la kupanga fedha hizo katika maeneo mbalimbali ni la Chuo chenyewe.

MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa mijibu wa bajeti ya Chuo cha Kilimo cha Sokoine, fedha wanazopata ni asilimia sitini mpaka sitini na tano ya mahitaji yao na fedha wanazopata kutokana na ruzuku ya Serikali, baada ya kutenga mahitaji muhimu yote unakuta hakuna fedha za utafiti. Fedha alizotaja Mheshimiwa Naibu Waziri, ni fedha za wafadhilli tu ambazo mara nyingine huwezi kuzitegemea sana. Je, wanawenza kuruhusu kama Chuo kikifanya *Supplementary Budget* kwa fedha za utafiti, wanawenza kuleta huku wakapata fedha za utafiti? Hilo la kwanza.

La pili, kama Wizara hii ndiyo inayosimamia mambo ya sayansi na teknolojia na utafiti ni moja katika sehemu kubwa sana ya kuendeleza sayansi na teknolojia. Je, Wizara inaridhika kwamba Chuo hakina fedha za utafiti za Serikali hata moja, wanaridhika hivyo? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Spika, nimeeleza kiasi cha fedha ambacho Chuo kimepata kwamba ni shilingi bilioni nne katika miaka minne. Nimeeleza vile vile kwamba katika fedha hizo kuna shilingi milioni thelathini ambazo zimetokana na kazi ambazo Chuo kimefanya. Fedha za utafiti bado ni fedha za Serikali, kwa hiyo, hizi pia ni fedha za Serikali ambazo zimetolewa. Hata hivyo, nimeeleza kwamba Chuo ndicho kinachopanga fedha katika maeneo yake mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali hairidhiki na fedha ndogo ambazo zimetengwa katika utafiti. Katika jibu langu la msingi nimesema pato la Serikali likiongezeka fedha zaidi zitapangwa. (*Makofî*)

MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swalii la nyongeza. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri lakini nilikuwa na swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inafanya kazi nzuri ya kuongeza mapato yake, lakini vile vile kwa sababu inapata msamaha wa madeni kwa zile nchi ambazo ni maskini na kwa kuwa sasa hivi Serikali imetoea kipaumbele kutoa fedha katika elimu ya msingi. Je, sasa Serikali inaweza kwa ujumla wake ikaangalia uwezekano wa kuongeza fedha katika Taasisi zetu za utafiti kama alivyosema mwenzangu ili tuweze kuongeza maarifa na teknolojia ili Taifa letu liweze kushiriki vizuri katika kukuza uchumi wake hasa katika enzi hizi za utandawazi; Serikali itakuwa tayari kuangalia uwezekano wa kuongeza fedha katika hizi taasisi zinazoshughulika na utafiti? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imesamehewa madeni, lakini haya ambayo yamesamehewa yanatakiwa kufanya shughuli mbalimbali katika Serikali yetu. Nimejibu kwamba pato la Serikali litakapoongezeka tutaongeza vile vile fedha katika fungu la utafiti. Serikali inatambua umuhimu wa tafiti mbalimbali ambazo zinafanyika na Wizara mbalimbali pia zinahusika na tafiti katika maeneo yake na mashirika mbalimbali vile vile yanahusika na tafiti mbalimbali katika maeneo yao. Hivyo basi, narudia tena kusema kwamba, pato la Serikali likiongezeka fedha zitaongezeka katika maeneo mbalimbali ya tafiti.

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa maana ya tafiti hasa hizi za kilimo ni kwa faida ya mkulima na Waziri amekiri kwamba fedha nyingi zinakwenda kwenye tafiti. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba yule mkulima anapata matokeo ya hizi tafiti kwa sababu kuna ma lalamiko ya namna hiyo kwamba tafiti hizi zinaishia huko juu haziwafikii wakulima?

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, juu ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya utafiti, naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Ngawaiya, kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi sana kwa ajili ya kuendesha vituo vya utafiti na wakulima wamekuwa wanakwenda moja kwa moja kwenye vituo hivi na watafiti wamekuwa wakiwatembalea wakulima na wamekuwa wakipata mafunzo kwenye Vyuo vyetu vya Kilimo. Kwa hiyo,

matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima moja kwa moja na tunaendelea kujitahidi kuimarisha utaratibu huu. (*Makofî*)

Na. 4

Matatizo ya Maji Wilaya ya Karagwe

MHE. ELIZABETH N. BATENGA aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe ni Wilaya yenye milima na ina matatizo makubwa ya maji:-

(a) Je, Serikali imefanya nini na itaendelea kufanya nini ili kupunguza shida ya maji kwenye Wilaya hiyo?

(b) Je, ni Kata ngapi hadi sasa bado zina matatizo ya maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalî la Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wilaya ya Karagwe bado ina matatizo ya maji. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa asilimia arobaini na tano ya wananchi wanaoishi katika Wilaya ya Karagwe, ndio wanaopata huduma ya maji safi na salama. Serikali kwa kushirikiana na wafadhili mbalimbali, imekuwa ikigharamia miradi ya maji katika Wilaya hiyo. Mipango ambayo imetekelezwa kwa miaka ya hivi karibuni ni pamoja na:-

- Mpango wa miaka mitatu (1996 - 1998) uliotekelizwa kwa msaada wa Serikali ya Ujerumanî;

- Mpango wa miaka miwili (1997 - 1998) uliotekelizwa kwa msaada wa Serikali ya Japan; na

- Mpango wa *HESAWA* uliokamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karagwe bado inaendeleza miradi ya maji kwa msaada wa Serikali ya Uhlanzi kupitia Programu ya Maendeleo ya Wilaya (*District Rural Development Programme*) na kupitia katika bajeti za Wilaya za kila mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karagwe inazo Kata 28, kati ya hizo Kata 15 zinapata maji safi kwa hali ya kuridhisha na Kata 13 hazipati maji safi kwa hali ya kuridhisha nazo ni Nyakahanga, Ihanda, Bugene, Igurwa, Kituntu, Kamuli, Rwabere, Kibongo, Ndama, Bweranyange, Nyakakika, Ihembe na Nyakasimbi.

Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe inapata mvua za kutosha, juhudi za kuwashamasisha wananchi ili wavune maji ya mvua zinaendelea. Kwa kuwa sera ya maji ni wananchi wenye kuandaa, kujenga na kuendesha miradi yao, namwomba Mheshimiwa Mbunge, akisaidiana na viongozi wenzake, aisaidie Serikali kuwashamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya watumiaji maji (*Water User Association*), ili wananchi waweze kupata maji safi na salama kwa juhudi zao. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutafuta fedha za ndani na nje ya nchi ili kusaidia kutatua tatizo la wananchi katika Wilaya na Kata alizozisema pamoja na maeneo mengine hapa nchini.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Kwa kuwa ni lengo la Serikali kuwawezesha wanawake na watoto ambao hasa ndiyo waathirika wakubwa wa maji, maana ndiyo wanaochota maji na kuyapata katika hatua fupi angalau mita mia nne kutoka nyumbani. Sasa katika jibu la msingi sikusikia kwa kweli kama kuna hatua za makusudi za kuweza kuwasaidia wanawake hao kupata maji safi. Lakini naomba ufahamu mpango uliopo angalau basi kwa Kata kama ya Nyakahanga ambayo ni jirani kabisa, ndani umo kuna Hospitali Teule ya Wilaya na Kata ya Kayanga, ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe kuweza kupata maji hayo angalau mwaka huu?

Pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba wananchi wahamasishwe kuvuna maji na kweli wananchi wa Karagwe wanayo juhudhi kubwa kujijengea matanki ya kuvuna maji, lakini Wizara inawasaidia vipi kuwapa wataalam ili waweze kupata maji yaliyo safi na salama kutokana na hayo maji ya mvua?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, maji yanahitajika siyo kwa wanawake na watoto peke yake, maji yanahitajika kwa binadamu wakiwemo wanawake, watoto, wanaume, mifugo na kadhalika. Kwa hiyo, jitihada za Serikali zinalenga kusaidia maeneo yote hayo ili kufikia lengo lake la upatikanaji wa maji wa mita mia nne kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema. Pia hii miradi niliyoisema inayoendeshwa na Serikali ya Uholanzi, vipaumbele vyta utekelezaji wa mradi huu vinafanywa kwa mapendekezo na ushirikiano mkubwa wa Halmashauri ya Wilaya. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya inaelewa ni maeneo yapi yenyenye matatizo makubwa na hiyo ikizingatia maeneo aliyojasema ya Kata ya Kayanga na Nyakahanga. Kwa hiyo, nina hakika kwamba maeneo hayo yote yatapatiwa ufumbuzi katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvunaji wa maji ya mvua katika eneo hilo, napenda nitoe pongezi kwa uongozi wa Wilaya ya Karagwe kwa vile ni kweli uvunaji wa maji ya mvua upo kwenye hali ya kuridhisha sana. Lakini naomba uongozi uzidishe bidii ya kuwashamasisha wananchi kuvuna maji ya mvua kwenye Wilaya hiyo na sehemu nyingine hapa nchini ili kupunguza matatizo ya maji ambayo yanatokana na umbali na matatizo ya vyanzo mbalimbali hapa nchini.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi Waziri amekiri kwamba, ni asilimia arobaini na tano wanaopata maji safi na kwa kuwa swali la msingi linazungumzia hali ya kijiografia ilivyo. Je, Mheshimiwa Waziri, yupo tayari kwenda Wilayani Karagwe ili aweze kuona hiyo milima ilivyo na jinsi ukosefu wa maji ulivyo ili aweze kuwashauri wataalam wake namna ya kwenda ku-*design programme* maalum kwa ajili ya kuvuna hayo maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba, nitakwenda Karagwe ili kuangalia *topograph* ya Wilaya hiyo lakini sitakwenda kwa nia ya utalii, nitakwenda kwa nia ya kuangalia matatizo ya maji.

Na. 5

Maji Lindi

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ (k.n.y. MHE. MARIA D. WATONDOHA) aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Lindi haupati maji salama na ya uhakika kwa muda mrefu sasa; na kwa kuwa wananchi hutegemea zaidi visima ambavyo maji yake si salama; na kwa kuwa Mamlaka ya Maji Lindi imeendelea kudai ankara za maji kwa mabomba ambayo hayatoi maji:-

- (a) Je, ni kwa msingi upi wananchi wanadaiwa kulipia huduma ambayo hawaipati?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika wa kuwaondolea kero wananchi wa Mji wa Lindi ili waweze kupata maji salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Maria D. Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mji wa Lindi una wateja wapatao 1,710 waliounganishwa kwenye mtandao wa mabomba. Mahitaji ya Mji wa Lindi kwa sasa hivi yanakisiwa kufikia lita 6,500,000 kwa siku, wakati maji yanayozalishwa kutoka kwenye vyanzo vilivyopo ni wastani wa lita 1,300,000 kwa siku. Kutokana na upungufu huo, wateja wengi hupata maji kwa njia ya mgawo na kiwango cha malipo ya mlingano (*Flat Rate*), kwa wateja walio wengi ndiyo kinachotumika. Kiwango cha chini kabisa kilichowekwa na Mamlaka ya Maji Lindi ni shilingi 2,400/= kwa mwezi.

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Mji wa Lindi imeanzisha utaratibu wa kufunga mita za maji ili kuhakiki matumizi ya wateja wake na uhalali wa malipo yao. Wateja wapatao 256 wamefungiwa mita za maji na wengi wao wanamudu malipo. Kwa msingi huo wateja wanalipa huduma wanayoipata na zoezi la kufunga mita linaendelea ili kuhakikisha kuwa wateja wanalipia huduma ya maji kulingana na huduma wanayoipata. Pale panapojoitokeza matatizo Mamlaka huweza kuyatatua.

(b) Ili kuwaondolea wananchi wa Mji wa Lindi kero ya upatikanaji wa maji, Serikali inatekeleza mradi wa dharura kwa ajili ya Mji huo. Mradi huo una lengo la kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 1,000 kwa siku hadi mita za ujazo 4,000 kwa siku ambazo ni sawa na lita milioni 4 kwa siku. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2001/2002 jumla ya shilingi milioni 61 zilitumika kununua mabomba na viungio, mitambo, dira za maji 150 na kuchimba kisima kimoja katika eneo la Mitwero. Kwa mwaka 2002/2003, Serikali imekarabati chanzo cha Liwayawayaya na kufunga mitambo mipya miwili ya kusukuma maji, pamoja na kuchimba visima virefu 6 eneo la Mitwero. Visima hivi vinatarajiwa kutoa zaidi ya mita za ujazo 800 kwa siku. Kazi nyingine zinazoendelea kwa sasa ni kuchimba visima virefu 5 katika eneo la Kitunda, ambavyo vinatarajiwa kuzalisha jumla ya mita za ujazo 2000. Pia, matengenezo ya bomba chini ya bahari yatafanyika hivi karibuni ili maji yapite kwenda Lindi Mjini, kutokea chanzo cha maji kilichoko baharini. Mradi huu unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 389. Sambamba na mradi huo, Wizara ilikwishanuna mabomba na viungio vyenye thamani ya shilingi milioni 25 katika mwaka huu wa fedha wa 2002/2003.

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Mji wa Lindi unapata maji chini ya asilimia 20 na kwamba Mradi wa Maji wa sasa ni mradi wa dharura; je, ni lini mradi wa kweli na wa kudumu wa maji kwa Mkoa wa Lindi utapatikana ?

(b) Kwa kuwa wananchi wa Lindi wana imani kubwa na Mradi wa Maji ya Ziwa Lutamba, ambalo lina maji mengi na ya baridi na ni ufumbuzi wa uhakika. Je, Serikali inasema nini kuhusu kuwapatia wananchi wa Lindi maji kutoka Ziwa Lutamba ambayo ni ya uhakika? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, jitihada mbalimbali zinafanyika kutatua tatizo la maji la Mji wa Lindi. Mji wa Lindi ulikuwa unapata maji yake kutoka kwenye chanzo cha maji kilichoko upande wa pili wa Bahari, kwenye mkondo unaoingia Mji wa Lindi. Lakini chanzo hicho kiliathirika baada ya bomba lake kupasuka na kuanza kuvuja ndani kwa ndani, kwa sababu ambazo haziwezi kuelezeka. Hivyo, baada ya bomba hilo kurudishiwa, pamoja na uchimbaji wa visima nilivyoitaja, mahitaji ya maji ya Mji wa Lindi ambayo nimeyasema ni *cubic* za ujazo 6,500 yataweza kutosheleza. Hivyo hivyo, bidii zitaendelea kupanua vyanzo vya maji mbalimbali ili kukidhi mahitaji yatakayofuatia katika kipindi kijacho kwa ajili ya Mji wa Lindi.

**Wizara za Serikali zinazofanya shughuli zake katika
Nyumba za Kupanga**

MHE. SALOME J. MBATIA aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi ni nafuu zaidi kufanyia shughuli katika nyumba yako kuliko nyumba ya kupanga:-

- (a) Je, ni Wizara ngapi zinafanyia shughuli zake katika majengo ya kupanga na kuanzia lini?
- (b) Je, Serikali imelipa fedha kiasi gani kwa mwezi na kwa mwaka kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita yaani mwaka 2000/2001 na 2001/2002 kwa upangaji huo?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa inapoteza fedha nyingi kwa kupanga badala ya kujenga au kununua majengo yake yenewe hasa ikizingatiwa kuwa sasa ni zaidi ya miaka 40 ya kujitawala?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya Wizara 16 zinafanyia shughuli zake katika majengo ya kupanga kuanzia vipindi tofauti kama ifuatavyo: Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Wizara ya Viwanda na Biashara. Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Afya, zinafanyia shughuli zake katika majengo ya *NHC*. Wizara nyingine ni Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, ambazo zinafanyia shughuli zake katika majengo ya *BIMA*.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka miwili iliyoulizwa kwenye swali (2000/2001 na 2001/2002), malipo ambayo Serikali imelipa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Jumla ya Sh.51,299,045/05 ni malipo kwa mwezi;
- (ii) Jumla ya Sh.615,588,540/60 ni malipo kwa mwaka; na
- (iii) Jumla ya Sh. 1,231,177,081/20 ni malipo kwa miaka miwili.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali inatumia fedha nyingi kwa kupanga badala ya kujenga au kununua majengo yake yenewe. Tatizo ni kuwa uwezo wa Serikali kupata fedha za kutosha kujenga au kununua majengo ya Ofisi zake zote ni mdogo. Hata hii itaweza kufikiwa wakati Serikali itakapokuwa na uwezo wa kupata fedha hizo kwa mara moja. Hata hivyo, sehemu kubwa ya majengo ambayo Ofisi za Serikali zinapanga ni majengo yaliyokuwa chini ya Shirika la Msajili wa Majumbaa, ambayo yalirudishwa Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*).

MHE. SALOME J. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali hivi sasa iko katika zoezi la kuuza baadhi ya nyumba zake; je, Serikali haioni kuwa ni busara kuzipa kipaumbele Wizara zake ambazo zinapanga?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali ipo kwenye zoezi la kuuza nyumba za kuishi kwa watumishi, haiuzi nyumba ambazo ni majengo ya ofisi na majengo ya ofisi maana yake ni nyumba moja inayoweza kuweka wafanyakazi 300 hadi 400. Kwa mfano, Wizara ya Ujenzi tuko wafanyakazi 400 katika ofisi. Kwa hiyo, huwezi kutumia nyumba ambazo wafanyakazi wa Serikali wanaishi. Lakini hata hivyo, tunajitahidi kwa kadri tuwezavyo kuweza kujenga nyumba hizo za ofisi siyo za kuishi.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kiwango cha malipo kilichotajwa ni kikubwa sana na kingeweza kujenga ofisi husika kwa kipindi kifupi sana. Je, Serikali sasa haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuamua kweli ili Serikali iondokane na gharama hizo kubwa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina mpango wa kujenga majengo kwa ajili ya ofisi zake. Lakini kama tujuavyo, kupanga ni kuchagua na katika mjadala uliopita imechaguliwa kujenga Jengo la Bunge kwanza badala ya Ofisi za Serikali. Kwa hiyo, katika mtiririko huo tunatoa kipaumbele kwanza kwa Waheshimiwa Wabunge, wajengewe jengo lao, halafu tutajenga nyumba nyingine za maofisi. (*Makofi*)

Na. 7

Kuundwa kwa Sekretarieti ya Mtwara
Development Corridor

MHE. RAYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa ni karibu miaka miwili imepita tangu Bunge liarifiwe juu ya umuhimu wa kuanzisha Kitengo au Sekretarieti inayojitegemea ya kuratibu, kufuatilia na kuharakisha kwa karibu Miradi ya Maendeleo ya Ukanda wa Maendeleo wa Kusini (*Mtwara Development Corridor*):-

- (a) Je, ni miradi au maendeleo gani ya kutia moyo ambayo yameletwa kutoptana na msukumo wa *Mtwara Corridor* kama Taasisi katika kipindi cha miaka miwili iliyopita?
- (b) Je, kwa nini Serikali haianzishi Sekretarieti au Kitengo cha Usimamiaji wa Maendeleo hayo kwa kuiga utekelezaji wa Mpango kama huo uliopo Msumbiji ambao unakwenda vizuri?
- (c) Je, ni nini hatma na mantiki ya usimamizi wa Ukanda huo kwa mujibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara (*Mtwara Development Corridor*), unajumu isha nchi nne wanachama wa SADC, ambazo ni Msambiji, Malawi, Tanzania na Zambia na ulianzishwa mwaka 1997 kuitia Tume ya Mawasiliano na Uchukuzi (*Southern Africa Transport, Communication and Meteorology Commission - SATCC*). Dhana ya kuanzisha Ukanda wa Mtwara kama ilivyo kwa Kanda zingine ni kuharakisha maendeleo kwa nchi husika kwa kutumia raslimali asilia (*Natural Resources*) ya eneo husika, ambapo miradi mbalimbali huainishwa kwa ajili ya uwekezaji. Kwa upande wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, hatua hii imeshafanyika na miradi mbalimbali ikiwemo miundombinu, nishati na madini, kilimo, utalii, viwanda na biashara na kadhalika imeshaainishwa.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna miradi yoyote ambayo imeanza moja kwa moja kutekelezwa chini ya Programu ya *Mtwara Development Corridor*, lakini kuna mafanikio ya kutia moyo kwa baadhi ya miradi miwili mikubwa (*Anchor Projects*), ambayo imepata wawekezaji. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma - Katewaka. Mradi huu unategemea kuzalisha megawati 400 za umeme na utagharimu Dola za Kimarekani milioni 600. Mradi huu unatarajiwa kuanza uzalishaji ifikapo mwaka 2006. Kwa sasa mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali na wawekezaji kuhusu namna ya kutekeleza mradi huu.

Mradi mwingine ni ule wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Mtwara-Masasi-Songea -*Mbamba Bay*, yenye urefu wa kilomita 829. Mradi huu umepata ufadhili kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*KUWAIT DEVELOPMENT FUND*), ambao unagharamia kazi ya upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*). Mtaalam Mshauri (*Consultant*) wa kufanya kazi hii alishateuliwa na tayari

ameshaanza kazi tangu mwezi Novemba, 2002. Kazi hii itachukua muda wa miezi tisa hadi kukamilika kwake na itagharimu Dola za Kimarekani milioni moja. Kwa kifupi, haya ndiyo mafanikio yaliyofikiwa hadi sasa. Aidha, kukamilika kwa miradi hii miwili kutachochea miradi mingine kutekelezwa chini ya programu hii.

(b) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huu wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, umekuwa ukisimamiwa na kuratibiwa chini ya Wizara ya Ujenzi, ikisaidiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*), ambayo pia imepewa dhamana na Serikali ya kusimamia na kuendeleza shughuli zote za miradi iliyopo kwenye Ukanda, ikiwa ni pamoja na kutafuta wawekezaji. Ni kweli ninakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna umuhimu wa kuanzisha Kitengo cha Usimamiji wa Maendeleo ya Programu ya *Mtwara Corridor (Technical Unit)*, kama vile ambavyo imekuwa ikifanyika kwa nchi ambazo zimeunda Kanda za Maendeleo.

Hata hivyo, mipango ya kuanzisha Kitengo hiki ndani ya Shirika la Maendeleo ya Taifa (*NDC*) inaendelea. Hadi sasa *NDC* imekwishapata msaada wa huduma za kitaalam wa kumwajiri Meneja wa Mradi, ambaye ataongoza *Unit* hii. Mtaalam huyu tayari ameshapatikana na ameanza kazi mapema mwezi Machi, 2003. Huyu ndiye atakayekuwa Mratibu wa shughuli za kitaalam zinazohusu *Mtwara Development Corridor*. Mtaalam huyu ametoka Malawi ambayo ni nchi mwanachama. Wizara ya Ujenzi itabakia kama Mratibu na Msimamizi kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano na Serikali na nchi wanachama. Nchi ya Msumbiji inatumia njia hii ya kuwa na Meneja wa Mradi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya Kanda za Maendeleo (*Development Corridors*).

Ni matumaini yangu kwamba, uanzishwaji wa Kitengo hiki katika Shirika la Maendeleo la Taifa na kuajiri Meneja wa mradi mahsus kwa ajili ya kuafuatilia na kuratibu shughuli za maendeleo ya *Mtwara Development Corridor*, utaharakisha kupata mafanikio na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Ukanda huu.

(c) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, kama ilivyo kwa shughuli zingine za maendeleo, inahusika kwa njia moja ama nyagine katika usimamizi wa Ukanda wa Maendeleo ya Mtwara, kwa sababu imekuwa ikifuatilia kwa karibu na kutoa maelekezo ili kuhakikisha kwamba, maendeleo halisi yanayotakiwa kupatikana kwa kutumia dhana hii mpya ya Kanda za Maendeleo yanapatikana.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pia kwa kufahamu kwamba *NDC* hiyo inayozungumziwa ndiyo iliyokuwa inashughulikia *Mtwara Corridor* kwa muda wote huu mpaka sasa, lakini hakuna chochote cha maana ninachokiona kutoka *NDC* kwa sababu ni Shirika moja lenye vitu vingi sana vya kushughulikia. Bado nauliza Serikali kwa nini isianzishe Sekretarieti itakayoweza kuhakikisha kwamba kuna maendeleo *Mtwara Development Corridor* na Mikoa mingine ya pembezoni ili kuwepo na maendeleo ya kweli?

(b) Kwa nini Serikali mpaka sasa inakuwa na kigugumizi cha maendeleo ya Mikoa hii ya pembezoni mpaka sasa tumekuwa na tatizo kubwa la barabara katika upande wa miundombini, Kibiti-Lindi ndiyo inaanza sasa hivi baada ya miaka 40, Songo Songo itaanza sasa hivi baada ya miaka 30; sasa kwa nini suala hili la Sekretarieti lisipewe kipaumbele ili kuweza kuleta maendeleo dhahiri yatakayoendeleza Mikoa hii baada ya vita ya *FRELIMO*?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI): Mheshimiwa Spika, kwanza *NDC* katika muundo wake mpya, jukumu lake kubwa sasa ndiyo hilo la kusimamia maendeleo katika mfumo wa *special development initiative*, ambayo mojawapo ni *Mtwara Development Corridor* na tuna nyagine ambazo ni *Central Development Corridor* na *Nothern Development Corridor*, zote hizi zinasimamiwa na *NDC*. Kwa hiyo, jukumu lake la sasa kwa *NDC* baada ya kuvuliwa mambo yake yote, kama tunavyofahamu Mashirika mengi yamebinafsishwa, hiyo ndiyo *function* ya *NDC* na hiyo kazi inaifanya vizuri sana mpaka sasa na ndiyo iliyowatafuta hawa wawekezaji wote kule Afrika Kusini na kwagineko. Kwa hiyo, hiyo ni kazi yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini swalii la pili kwamba Serikali ina kigugumizi kuhusu maendeleo ya Kusini siyo kweli. Daraja kubwa katika nchi yetu na katika Afrika limejengwa katika Mto Rufiji, ambalo linaunganisha nchi yetu na sehemu ya Kusini ya nchi yetu. (*Makofifi*)

WABUNGE FULANI: Barabara!

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI): Pili, barabara ya lami itakayojengwa au ilishaanza kujengwa kati ya Dar es Salaam na Mtwara inakwenda kule kule, kama sehemu ya *Corridor* kuna barabara itajengwa Mtwara-Masasi-Tunduru-Songea mpaka *Mbamba Bay* na hiyo barabara ni kama sehemu ya *Corridor* tunaifanya kazi kubwa. Kwa hiyo, hakuna suala la kuwa na kigugumizi katika Serikali hii kwa ajili ya maendeleo ya Kusini. (*Makofifi*)

Na. 8

Nyumba za NHC Zinazouzwa

MHE. MARIAM S. MFAKI aliuliza:-

Kwa kuwa wapangaji wa nyumba za *NHC* walipewa taarifa kuwa tarehe ya mwisho ya kuuziwa nyumba ni tarehe 30 Juni, 2003 ili wasioweza kununua waondoke; na kwa kuwa wapangaji hawa wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu wakiomba Serikali iwasaidie mambo yafuatayo kutokana na uwezo mdogo walionao; yaani kupunguza kiwango cha kuanza kulipa, kuongeza muda wa kulipa badala ya mwaka mmoja na kuwauzia wanaoishi katika nyumba hizo: Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu wananchi hawa maana wanahofia kuadhirika watakapotolewa kwenye nyumba hizo?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali iliwapo muda wapangaji wa Shirika la Nyumba la Taifa katika nyumba zilizomo kwenye mpango wa kuuzwa, yaani nyumba ndogo ndogo na za kati, kulipia nyumba hizo hadi tarehe 30 Juni, 2003. Baada ya tarehe hiyo, wapangaji watakaoshindwa kuzilipia watatakiwa waondoke ili nyumba hizo ziuzwe kwa Watanzania wanaopenda kuzimiliki. Tamko hilo la Serikali linaendelea kutekelezwa na wapangaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina sababu ya kupunguza kiwango cha kuanza kulipa kwa kuwa muda uliotolewa unakaribia kumalizika. Hata hivyo, kiwango cha kuanza kulipa kinachotumika hivi sasa cha asilimia 25 ya bei ya nyumba kimeweza kulipwa na wapangaji wengi. Hadi tarehe 31 Machi, 2003 wapangaji zaidi ya asilimia 63 walikuwa wamekwishalipia kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, siyo sahihi kuwa wapangaji walipewa mwaka mmoja kulipia nyumba zao. Ukweli ni kwamba, Serikali iliwaruhusu kuzinunua tangu mwaka 1993. Ni wazi kuwa, wapangaji hao walikuwa na muda wa miaka 10 kuweza kuzilipia nyumba hizo. Hivyo Serikali inaona muda huo unatosha kwa mpangaji aliyedhamiria kununua nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuwauzia nyumba ndogo na za kati za Shirika wapangaji wanaoishi katika nyumba hizo ni uamuzi wa Serikali. Katika utekelezaji wake Shirika la Nyumba la Taifa linawauzia wapangaji wanaoishi kwenye nyumba ndogo ndogo na za kati kwa bei nafuu kabisa. Baada ya wapangaji wanaoishi kwenye nyumba hizo kushindwa kuzinunua, ndipo watauziwa wananchi wengine kwa bei ya soko.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika jibu lake ameeleza kwamba baadhi ya wapangaji wengi wamelipa na walio baki ni wachache:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapangaji hao inawezekana ni wachache, lakini hao wachache ndiyo mpaka sasa bado wanalamika kwamba uwezo wa kiwango cha kulipia cha mwanzo ni kikubwa, halafu vilevile maombi yao ni haya ya kupunguziwa muda na kile kiwango cha kwanza cha kulipa. Sasa Serikali bado inaendelea kusisitiza kwamba wale ambao hawatalipa wataondolewa kwenye nyumba hizo na watauziwa watu wengi. Serikali haioni kwamba kuwaondoa watu ambao wameishi katika nyumba hizo kwa muda mrefu ni kuwafanya waadhirike au waonewe na kwamba wanawenza wakakosa imani na Serikali yao?

(b) Kuna tatizo gani kubadilisha hivyo viwango au muda wa kulipia ili kuwawezesha hao walioishi muda mrefu katika nyumba hizo waweze kuzinunua, kwa sababu wengine mpaka wamejukuu katika nyumba hizo, sasa kumwondo mtu kama huyo ni kumwonea? Mimi naomba Serikali iwe na imani na watu hawa. Naomba majibu. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa muda waliopewa wapangaji wa miaka 10 kwa mwenye nia angekuwa amejiandaa. Lakini kama ilivyokuwa katika ulipaji wa viwanja 20,000 vya sasa tulivyopima Dar es Salaam, walipewa muda mrefu, lakini siku ya mwisho karibu ngazi zikatike kwa ajili ya kulipia. Kwa hiyo, tumekuwa na tabia ya kupuuzia maelekezo ya Serikali kwamba, miaka 10anza kujandaa, lakini bado mwezi mmoja muda uishe ndipo anakuja kusema mimi siwezi kulipa, mimi ni mpangaji wa siku nydingi, kweli wewe ni mpangaji siyo nyumba yako ni nyumba ya Serikali. Aidha, unajiandaa kujenga nyumba yako mwenyewe au kama unaendelea kuwa mpangaji basi ufuate maelekezo ya Serikali. Zile nyumba ni za Serikali siyo nyumba za mtu binafsi, Shirika pia likikodisha linapeleka fedha hizo kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa hiyo, ni moja ya mchango wa fedha katika mfuko wetu wa Hazina.

Sasa kuhusu kubadilisha kiwango, nyumba zinakwenda kwa thamani, zilikuwa na thamani ndogo wakati walipokuwa wanaanza, sasa siku zinavyokwenda ndivyo thamani yake inavyozidi kukua. Sasa tukisema kwamba tuanze upya tena turudi nyuma, mambo mengi yatarudi nyuma basi hata Serikali haitaendelea. Kwa hiyo, naomba tuwaelimishe wapangaji wetu kwamba muda umekwisha. Kuna matatizo ya mtu mmoja mmoja, unajua kabisa kwamba huyu ana matatizo, bado tunaweza tukazungumza, lakini siyo kupunguza kiwango wala kuongeza muda.

Na. 9

Upimaji wa Viwanja Dar es Salaam

MHE. SOPHIA M. SIMBA aliuliza:-

Kwa kuwa mpango wa upimaji wa viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam una malengo mazuri sana yakiwemo yale ya kupunguza ujenzi holela, uharibifu wa mazingira, pamoja na kurahisisha uwekaji wa miundombinu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kwa kuwatoza wananchi kiwango kikubwa cha ununuzi wa viwanja hivyo kwa kiasi cha chini cha Sh. 500,000/= kuwa ni bei kubwa sana na hakiwalengi wananchi wenye kipato kidogo hivyo kusababisha wananchi hao kuanzisha *squatters* nyingine?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba sasa wale wananchi wanaoshindwa kununua viwanja hivyo wanakimbilia maeneo ya mabondeni na hivyo kuendelea kuharibu mazingira?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam umeghamariwa na Serikali kwa kutumia shilingi bilioni 8.9 kama mkopo wa shughuli zote za Mradi, ambazo ni pamoja na uthamini, ulipaji wa fidia ya mali za wananchi ndani ya maeneo ya mradi, fidia ya thamani ya ardhi, uandaaji wa michoro na mipango miji, upimaji wa viwanja na uwekaji wa miundombinu

kwa mfano barabara. Wizara yangu haina budi kurejesha fedha hizo kwa utaratibu wa kuchangia gharama kwa watakaopewa viwanja hivyo. Viwango vinavyotozwa kwa viwanja vilivyopimwa chini ya Mradi huu, kama vile shilingi 500,000 na kadhalika, vinatokana na gharama halisi ya uzalishaji wa viwanja.

Aidha, azma kubwa katika zoezi la kupima viwanja ilikuwa kutatua tatizo la uhaba wa makazi. Ili kutekeleza azma hiyo, viwanja vinavyopimwa vinagawiwa kwa watu wenye uwezo na sifa zinazotakiwa ili waweze kujenga. Kama mtu atashindwa kutoa shilingi 500,000/= hata uwezo wake wa kujenga ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, hakuna wananchi waliokuwa wakiishi katika eneo la Mradi walioshindwa kununua viwanja na kuhamia maeneo mengine na kuanzisha makazi yasiyo rasmi, Serikali haina taarifa hizo wala Halmashauri za Wilaya hazina taarifa hizo. Suala hili lilizingatiwa wakati wa kubuni mradi, hivyo, maeneo mengi ya mradi ni yale yaliyokuwa yanatumiwa kwa kilimo. Nyumba chache zilizokutwa, ziliingizwa kwenye viwanja ili wenye nyumba hizo waendelee kumilikishwa viwanja hivyo. Nyumba ambazo ziliangukia barabarani au katika maeneo ya matumizi maalum, watusika walilipwa fidia na kuvunjwa ili kuendana na matumizi yaliyopangwa kwenye mpango wa makazi na wenye nyumba hizo wamepewa viwanja mbadala ndani ya eneo la mradi.

(b) Mheshimiwa Spika, moja ya malengo ya Mradi wa Upimaji Viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam ni kupunguza matatizo yanayotokana na ujenzi holela na hasa katika maeneo hatari kama vile mabondeni. Katika utekelezaji wa Mradi huu, hakuna mwananchi aliyekuwa na nyumba katika maeneo hayo ambaye hakupata kiwanja. Hivyo, hakuna wananchi waliokosa viwanja na waliokimbilia kujenga mabondeni. Ni muda mfupi mno kutoa tathmini kwamba baada ya upimaji wa vile viwanja katika muda wa miezi minne, watu wamekimbilia mabondeni, si kweli. Kama wapo Wizara yangu iko tayari kuwasaidia kwa kufuata taratibu za mradi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, pamoja na upimaji wa viwanja katika eneo la Mradi, pia Halmashauri za Manispaa zote tatu za Ilala, Temeke na Kinondoni, zinaendelea kupima viwanja kwa ajili ya wananchi wa kawaida. Upimaji kutoka pande zote mbili utapunguza sana ujenzi wa nyumba mabondeni au ujenzi holela. Natoa wito kwa mamlaka zinazohusika, kusimamia kikamilifu Sheria za Ardhi na Makazi ili kulinda mazingira ya sasa na baadaye.

MHE. SOPHIA M. SIMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa uwezo wa kulipia viwanja hivyo ni mdogo kwa wananchi wengi na hata wale ambaao wamelipwa fidia katika maeneo hayo wengi wameshindwa kuvilipia tena; kwa kuwa viwanja hivyo ni mashamba ambayo yalikuwa ni ya ukoo; na kwa kuwa wengi wameshindwa kulipia hasa katika maeneo ya Kata za Tuangoma, Kisota, Mjmwema, Kimbiji, Mbweni, Bunju na kadhalika; na kwa kuwa wengi waliopatiwa viwanja hivyo sasa wanatembea na fomu wanashindwa kwenda kulipa; na kwa kuwa hakuna utaratibu mzuri wa kuwawe zesha kulipa kwa muda mrefu: je, Serikali ipo tayari kuweka utaratibu wa kuweza kulipia viwanja hivi kwa *instalment*, utaratibu ambaao uko wazi tofauti na utaratibu ule ambaao sasa hivi watu wanakwenda Wizara ya Ardhi kujaribu kupata kibali ili walipe kwa *instalment*?

(b) Je, Serikali chini ya sera nzuri za Chama cha Mapinduzi, ina utaratibu gani wa kupima viwanja vingi zaidi, vyatengenezwa ili kukidhi hamu ya ujenzi wa wananchi wengi katika miji yetu hapa nchini? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Mheshimiwa Sophia Simba na yeze pia ni mkazi wa Tuangoma ndiyo maana anafuatilia sana. Lakini naendelea kusema kwamba, si kweli, wengi wamelipwa viwanja. Kwa hiyo, siwezi kusema kwamba muda hautoshi, uwezo hawana, wale wengi ambaao wamechukua viwanja kule wana uwezo isipokuwa kama ninavyosema kwamba, wanasinzia wenywewe ndio maana wameona ile foleni katika

wiki za mwisho wamekuwa wengi. Ndiyo hayo ninayosema kutoka Wizarani. Kama mtu amekuja kuzungumza au kutazama tazama hakuwa na uhakika, mimi ndiye ambaye nafuatilia sana katika malipo hayo na yanafanyika katika ghorofa ambayo nafanya kazi.

Wengi waliochukua vile vibali wanaviuza, amechukua kibali ili amuuze mtu ambaye ana uwezo zaidi. Lakini waliolipa kidogo, robo au nusu hatujawakatalia wamelipa. Tumeweka utaratibu maalum ambao tumefanya sensa ya kutosha kwamba wale watu wasio na uwezo na wana nia kweli wameanza kupewa nafasi ya kulipia angalau nusu, wakapewa muda kipindi kidogo wakachangia. Hakuna mtu aliyefukuzwa aliyekuwa na fedha kidogo, kama amefukuzwa basi naomba aniletee majina mimi nitafuatilia. (*Makofi*)

Lingine la kusema kwamba kupima maeneo mengine kwa gharama kidogo, inategemea Mipango Miji. Tunapima kutokana na maandalizi yaliyopo. Hatuwezi kuwa tunapima ovyo ovyo, tumepima hivi ili kupanua Mji wa Dar es Salaam, lakini bado hata vijiji vingine vitaendelea kupimwa kutokana na matakwa ya maeneo hayo. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Nawaona wanaotaka kuuliza maswali ya nyongeza lakini muda wa maswali umekwisha.

Kabla hatujaendelea, kuna matangazo ya vikao vya Kamati kwa leo. Kamati zinazotambuliwa na Kanuni za Bunge, Kamati ya Wabunge wote wa CCM watakuwa na kikao mara baada ya kusitis ha shughuli za Bunge asubuhi hii, wakati wowote ule tutakapomaliza shughuli za Bunge, Kamati ya Wabunge wa CCM watakuwa na kikao. Hali kadhalika Kamati ya Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani na wao vile vile tukishasitisha shughuli za Bunge na wao watakuwa na kikao.

Mwisho wa matangazo.

TAARIFA ZA KAMATI

SPIKA: Mheshimiwa Simpasa, ameniarifu kwamba anazo taarifa mbili. Nitamwomba aziwasilishe moja baada ya nyingine ili ziweze kujadiliwa kwa pamoja.

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu Tuhuma zilizotolewa na Mheshimiwa Phillement Ndesamburo Bungeni

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, naomba kuwasilisha taarifa mbili zifuatazo: Ya kwanza, ni Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu tuhuma zilizotolewa na Mheshimiwa Phillement Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, walioshughulikia kazi uliyoipangia ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Mwalimu Eliachim J. Simpasa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba - Mjumbe, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed - Mjumbe, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi - Mjumbe, Mheshimiwa Cynthia Ngoye - Mjumbe, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga - Mjumbe, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah - Mjumbe, Mheshimiwa Maria Watondoha - Mjumbe na Mheshimiwa Bernard Membe - Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilikuwa na Makatibu wafuatao: Ndugu Charles Mloka na Bi. Nenelwa Mwihambi

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, Mheshimiwa Phillement Ndesamburo, alipokuwa akichangia mawazo yake Bungeni, wakati wa mjadala wa Muswada wa Sheria ya *The Fair Competition Bill, 2003*, alitoa madai yafuatayo kwamba: "Mfanyabiashara ukitaka mambo yako yakunyookee sharti

uingie CCM, ili ufanye biashara usiguswe na *TRA* ni lazima uingie CCM na sisi wengine hapana.” (*Hansard* ya tarehe 2 Aprili, 2003 uk. 50 aya ya mwisho).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(9) ya Kanuni za Bunge, uliandikia Kamati yangu barua Kumb. Na. BD/50/155/05, ukiiagiza ufanyike uchunguzi wa maelezo binafsi, ambayo yaliwasilishwa mezani kwako kama ulivyokuwa umemtaka afanye hivyo kwa mujibu wa Kanuni Na. 50 ya Kanuni za Bunge kwamba, Kamati ione kama kweli maelezo hayo yamethibitisha tuhuma alizozitoa awali Bungeni, kwa kiwango cha kuridhisha Bunge na hatimaye kutolewe taarifa kwa Spika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo, Kamati yangu tarehe 9 Aprili, 2003 iliketi na kuchambua kwa kina ushahidi uliotolewa na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo. Kamati yangu kwa kauli moja ilibaini kwamba, ushahidi wa Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, haukuthibitisha madai yake kwa sababu zifuatazo:-

1. Alishindwa kutoa waraka wowote wa Serikali au wa Baraza la Mawaziri ulioagiza wafanyabiashara wa CCM wapendelewe kwa namna yeoyote ile;
2. Ushahidi wa magazeti alioutoa hauthibitishi kwa sababu magazeti sio kauli ya Serikali na kila mmoja anaandika kadri ya mtazamo wake, kama tunavyoona wote hapa;
3. Ameshindwa kuthibitisha ni mfanyabiashara yupi ambaye ni mwana CCM aliyependeleta na *TRA* kwa namna moja au nyininge;
4. Ameshindwa kuthibitisha ni mfanyabiashara yupi wa Chama cha Upinzani ambaye amesakamwa na *TRA*, wapi na lini, hajathibitisha; na
5. Vielelezo vyake vyote havionyeshi popote kwamba Waziri Mkuu, alitoa agizo kwamba mfanyabiashara wa CCM apendelewe au asifuatwe na *TRA* na kwamba mwingine yeoyote asakamwe.

Kwa kuwa Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, katika kujibu hoja yake, ameshindwa kuthibitisha chochote, Kamati yangu imeona kwamba, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, amekiuka Kanuni Na. 50(1) mara mbili, tarehe 2 Aprili, 2003 (*Hansard* Uk. 50) na tarehe 7 Aprili, 2003 (*Hansard* Uk. 48), pale alipokataa kwamba aliituhumu *TRA* na pia amekiuka Kanuni 50(8)(d) kwa kuleta malumbano ya kisiasa Bungeni. Kwa kuwa hii ni mara ya pili anatoa madai ya uwongo, ya kwanza aliyatoa tarehe 27 Machi, 2001, wakati akichangia Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ya mwaka 2000. Kama Msemaji Mkuu wa Upinzani, alidai kwamba, nanukuu: “Mimi natoa mfano, mimi ni Mpinzani, nilichaguliwa kutoka Chama cha Upinzani, lakini kwa bahati mbaya au sijui bahati nzuri, nina mtoto alikuwa anafanya kazi Serikalini na siyo pengine ni *Treasury* na ni msomi mzuri tu, amefukuzwa kutoka *Treasury* kwa sababu baba yake yuko *Opposition*.” Tuhuma hii ilijibowi na Waziri wa Fedha tarehe 4 Aprili, 2001 na kuthibitika kwamba binti yake hakufukuzwa kazi bali alirudishwa kufundisha Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam, alikokuwa Mwalimu pale, ndipo alipokuwa mwajiriwa mara ya kwanza mwaka 1982.

Kwa kuwa Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, katika kujibu hoja alitoa malumbano ya kisiasa Bungeni, kuwavunja heshima Waziri Mkuu na Spika wa Bunge, kuzusha hisia mbaya mionganoni mwa Watanzania kwa maneno ya uzushi na kwa kuwa Tanzania ni nchi ya Demokrasia ya Vyama Vingi, lakini kwa kuwa hakuna demokrasia ya kweli bila nidhamu, kwa mujibu wa Kanuni Na. 60(3) na Kanuni 61, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, apewe adhabu ya kutohudhuria Bunge kwa kipindi chote cha Mkutano wa 12 wa Bunge lako Tukufu. Lengo letu ni kujenga nidhamu katika Bunge, kuleta utulivu, maelewano na mshikamano wa kujenga nchi yetu na siyo malumbano ya kisiasa ndani ya Bunge. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, tunasisitiza lengo la chombo chako kitukufu, kamwe Bunge lisije likageuzwa kama klabu ya masuala ya kisiasa. Bunge siku zote na Wabunge wote kwa ujumla, tujielekeze katika hoja za kujenga nchi yetu ya Tanzania na si vinginevyo. Mwandishi mmoja wa hadithi katika Essopo anasema: "Usidharau mambo madogo haifai kuyapa kisogo". Tukiacha tabia hizi za uzushi, uongo, ziendelee na kushamiri Bungeni, nchi yetu itayumba na wananchi wetu watakosa imani kwa Wabunge wao na Bunge lenyewe kama chombo chao na sauti yao. Demokrasia bila nidhamu siku zote ni fujo na ni vurugu. Tabia ya Mbunge yejote kuwa mwongo ni mbaya na inastahili kukemewa kwa adhabu kali.

Mheshimiwa Spika, tulipendekeza kuanzia leo Mheshimiwa Ndesamburo, asihudhurie kipindi chote cha Bunge hili lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu Tuhuma ya Kumsamehe Deni
Mama Saada Kitine iliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali**

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu uchunguzi juu ya maamuzi ya kufuta hoja ya Mama Saada H. Kitine na kusamehe deni la Serikali la Dola za Kimarekani 63,450, kiasi cha shilingi milioni 63.4.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, taarifa rasmi ya Kamati hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(ii) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inawasilishwa mbele ya Bunge hili kwa mujibu wa barua zako mbili ulizozipeleka kwenye Kamati yangu, barua ya tarehe 2 Aprili 2003 na barua ya tarehe 22 Mei, 2003, uchunguzi wa tuhuma ndani ya barua hizo unawalenga dhahiri Waheshimiwa wafuatao:-

1. Mhe. Richard Ndassa;
2. Mhe. Dr. Amani W. Kabourou; na
3. Mhe. Dr. Hassy H. B. Kitine.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kwamba, licha ya Waheshimiwa hawa watatu, kila mtu aliyesikika kwa njia moja au nyininge na tuhuma hiyo, alifika mbele ya Kamati na *Hansard* ipo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niwatambue na niwataje kwa majina Wajumbe wa Kamati waliohusika na kuchambua tuhuma hiyo. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Mwalimu Eliachim J. Simpasa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Maria Watondoha - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Chifu Abdallah S. Fundikra - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai - Mjumbe, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed - Mjumbe, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Mjumbe, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba - Mjumbe, Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo - Mjumbe, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah - Mjumbe, Mheshimiwa Juma S. N'hunga - Mjumbe, Mheshimiwa Abdullatif H. Esmail - Mjumbe, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono - Mjumbe, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi - Mjumbe, 2002, ulionyesha kwamba, Wajumbe wafuatao ndio waliohudhuria kikao hicho, naomba nao pia niwasome kwa idhini yako.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe waliohudhuria ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Richard Ndassa, - Kaimu Mwenyekiti, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah - Mjumbe, Mheshimiwa Issa Mohamed Salim - Mjumbe, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa - Mjumbe, Mheshimiwa Ernest G. Mabina - Mjumbe, Mheshimiwa Lephy Gembe - Mjumbe, Mheshimiwa Estherina Kilasi - Mjumbe, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte - Mjumbe, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo - Mjumbe, Ndugu Elisa D. Mbise - Katibu wa Kamati, Ndugu Emanuel Shuli - *Assistant Controller and Auditor General*, Ndugu C. M. Mbawala - Mkaguzi, Ndugu H. A. Minja - Mkaguzi, Ndugu H. H. Kagaza - Mkaguzi, Ndugu Andrew Mzikila - Afisa wa Hazina, Ndugu Ezra Msanya - Afisa wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wafuatao hawakuhudhuria kikao hicho: Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou, Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira, Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Paul N. Makolo na Mheshimiwa John L. Mwakipesile.

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza kwa mujibu wa muhtasari wa Kikao cha *PAC* cha dharura cha tarehe 14 Februari, 2003, ni kama ifuatavyo:-

- (i) Wajumbe wote walikubali kujadili hoja ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kuhusu Hesabu za Fungu 46, tarehe 19 Julai, 2002, wote walikubali na wanasema ndio iliyojitokeza kwa *PAC* siku hiyo;
- (ii) Wajumbe wengine wote walikana kabisa kujadili hoja inayohusu Deni la Mama Kitine kwamba lilikwisha jadiliwa kasoro Mheshimiwa Ndesamburo na Mheshimiwa Ndassa;
- (iii) Wajumbe wawili kwanza Mheshimiwa Estherina Kilasi na baadaye Mheshimiwa Jere miah J. Mulyambatte, walikana kuhudhuria kikao hicho cha tarehe 19 Julai, 2002, kwa hiyo, waliandikwa tu; na
- (iv) Kamati ilimwagiza Katibu wa Bunge kuwaandikia wahusika kufuta maagizo ya Kamati yaliyotolewa tarehe 19 Julai, 2002 kuhusu hoja ya Mama Kitine.

Kwa kuwa tukio hilo lilitokea katika mazingira yenye utata na njia zisizo za kawaida, kwa mwenendo na Kanuni za Bunge, Kamati hiyo tarehe 14 Februari, 2003, ilipendekeza kwa Mheshimiwa Spika kwamba, wote waliohusika kwenye kikao hicho, wapelekwe mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili heshima ya Bunge ilindwe. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza pendekezo la Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, uliandikia Kamati yangu barua, kuitia kwangu kama Mwenyekiti, ukiagiza ifanye uchunguzi juu ya suala hilo na kulitolea taarifa kwa Spika ipasavyo. Katika barua yako ya tarehe 2 Aprili, 2003, kama nilivyosema huko nyuma, ulimtaja Mheshimiwa Ndassa, kama mtuhumiwa katika kikao hicho cha Kamati kwamba, Mbunge huyu akiwa Mwenyekiti wa Muda wa Kikao cha Kamati kilichofanyika siku hiyo ya tarehe 19 Julai, 2002, alifanya mambo yafuatayo ambayo ni kinyume kabisa na taratibu za vikao vya Kamati hii:-

- (i) Kwamba alisaini kumbukumbu za kikao hicho na kuzipeleka kwa Katibu wa Bunge kabla hazijathibitishwa na Kamati hiyo, ye ye peke yake akishirikiana na Katibu wa Kamati hiyo na kwamba alisaini kumbukumbu hizo nje ya kikao katika maeneo ya kantini ya Bunge; na
- (ii) Kwamba ndani ya kumbukumbu hizo alizozitia saini, kulikuwa na mambo ya kugushi yafuatayo:-
- Kati ya Wajumbe tisa walioonyeshwa katika orodha ya Wajumbe waliohudhuria kikao cha siku hiyo, mmoja wao amekana kuhudhuria kikao hicho. Sasa ni wawili, kwa sababu na Mheshimiwa Mulyambatte naye alikataa kwenye kikao chetu na ilithibitika;
- Hata Wajumbe waliohudhuria kikao cha Kamati hiyo tarehe 19 Julai, 2002 walikana kwamba *agenda* ya kumsamehe Mama Saada Kitine, asilipe deni analodaiwa na Serikali la *USD 63,450* ilijadiliwa na kukubaliwa; na
- Kwamba kumbukumbu alizozitia saini zilikuwa na maamuzi ambayo Kamati haina uwezo wa kufanya, yaani uamuzi wa kusamehe malipo ya deni la Serikali, Kamati haina uwezo huo.

Mheshimiwa Spika, katika barua yako ya pili ya tarehe 22 Mei, 2003 ulielekeza na kusisitiza kwamba, Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou na Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, pia wafike mbele ya Kamati yangu kwa kuwa ilibainika katika mwenendo wa majadiliano kwamba ni wahusika wakuu.

Mheshimiwa Spika, jinsi Kamati ilivyofanya kazi yake, Kamati iliwaita na kuwahoji watuhumiwa, mashahidi ndani na nje ya Ofisi ya Bunge, kwa mfano, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Wizara ya Fedha. Kamati pia ilipitia nyaraka mbalimbali za mawasiliano kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Mama Saada Kitine, mawasiliano kati ya Mheshimiwa Dr. Kabourou na Mama Kitine, muhtasari wa vikao vya *PAC* vyote viwili, *Hansard* ya tarehe 6 Machi, 2002, vyote tulivipitia. Aidha, Kamati ilipoona ukweli unajifichwa au kuna utata wowote, ililazimika kuwakutanisha wahusika wote wawili au watatu kwa pamoja ili kila mmoja asikie yale ambayo mwenzake alikuwa ameshaiambia Kamati. Jambo hili lilfurahisha sana, maana ilifika mahali watu wakaanza kutazamana hawawezi kuongea.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikwishakutana na Wajumbe wa zamani na wapya wa Kamati ya zamani, ambao nao walikana kabisa *agenda* hiyo kujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, kazi uliyotupa ilikuwa ngumu sana, nikisema hivyo inaeleweka, lakini Kamati yangu kwa moyo na kwa uadilifu mkubwa sana, imeikabili na kuikamilisha kazi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wetu ulizingatia hadidu za rejea ulizotupatia kwa mujibu wa barua zako zote mbili. Kamati ilibaini hoja tatu baada ya kukutana na wahusika. Hoja hizo ni:-

- (i) Uhalali wa Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*) kilichoketi tarehe 19 Julai, 2002. Uhalali wake je ni halali;
- (ii) Utaratibu uliotumika katika kujaribu kuondoa hoja ya deni la Mama Kitine na uamuvi wa kumrejeshea fedha ambazo tayari ameshalipa; na
- (iii) Yaliyojitekeza kutokana na hayo mawili ya juu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha maoni ya Kamati yangu kwa kila hoja, kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Uhalali wa kikao cha tarehe 19 Julai, 2002, Kamati ilipokea ushahidi kuhusu kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali cha tarehe 19 Julai, 2002 kama ifuatavyo:-

- (a) Kwanza, kikao cha *PAC* cha tarehe 19 kiliitwa maalum kujadili suala la kompyuta zilizonunuliwa na Wizara ya Elimu na ununuzi wa magari kutoka *KJ Motors*. Hii ndio sababu wataalam wa Wizara ya Elimu tu walihudhuria kikao hicho. *Agenda* ya deni la Mama Kitine haikuwepo kama ingekuwepo wataalam wa Wizara ya Afya wangelikuwepo;
- (b) Kati ya Wajumbe wote wa *PAC* waliota ushahidi, ni mmoja pekee, ambaye ni Mheshimiwa Ndesamburo, ndio anasema ilijadiliwa. Kamati haiwezi kumwamini mtu mmoja kati ya watu 16;
- (c) Mwenyekiti wa muda wa Kamati hiyo kwa tarehe hiyo 19 Julai, 2002, Mheshimiwa Richard Ndassa, aliambia Kamati kuwa *agenda* hiyo ilijadiliwa kutokana na maagizo aliyyoyatoa Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, wakati anamtaka akaimu Uenyekiti, lakini Mheshimiwa Kabourou, alipofika alikanusha vikali na alikana maelezo hayo; na
- (d) Mheshimiwa Richard Ndassa, alikubali kuwa alisimamia uandishi au uhariri wa kumbukumbu za kikao hicho yeye mwenyewe. Aidha, alitoa maelezo kuwa inawezekana Wajumbe walionyeshwa waliohudhuria na wakaonekana hawahudhurii kwa sababu kuna tabia ya watu wengine kuandika majina kule

ya wenzao ili wapate posho. Hata hivyo, ilibainika kuwa kikao kilifanyika wakati wa Bunge la Bajeti, kwa hiyo, hakukuwa na kulipwa posho. Hoja hiyo ilitupwa kando.

(e) Mheshimiwa Spika, ushahidi uliotolewa na kukubalika kuwa Mheshimiwa Kilasi na Mheshimiwa Mulyambatte hawakuhudhuria kikao ulithibitishwa.

(f) Kuwa, mara baada ya Mheshimiwa Bernard Membe kuwasilisha maelezo yake binafsi Bungeni, *PAC* ndipo ilizinduka na bila kibali rasmi kutoka kwa Spika ikaamua kukutana kwa dharura.

(g) Kamati ilitazama *note book* ya Bwana Mbise aliyokuwa akichukulia mjadala wa kifungu cha 46 cha Wizara ya Elimu, haikuona suala la Mama Kitine kujitokeza.

(h) Mheshimiwa Ndassa na Katibu Ndugu Mbise; Katibu wa Kamati walisema kuwa suala la Mama Kitine halikuchukua hata zaidi ya dakika kumi, licha ya uzito wa jambo lenyewe, ilichukua kama dakika tano/sita, wamemaliza! Hii inahalalisha kwamba suala hilo halikujadiliwa. (*Kicheko*)

(i) Ushahidi ulitolewa kuwa muhtasari ulioandalishi uliandikwa baada ya Katibu wa Bunge kuomba kwamba: “Kama maamuzi ni hayo basi naomba sahihi za wahusika” na ndipo pale Mheshimiwa Ndassa pamoja na Katibu wake walipokwenda kusaini muhtasari huo *canteen*.

(j) Kwamba kwa kawaida hapakuwa na utaratibu wa kuandika kumbukumbu za vikao hivyo vya *PAC*. Maoni ya Kamati kuhusu haya tuliyosema ni kwamba:-

(i) Hoja ya kuondoa hoja ya deni la Mama Kitine na kumrejeshea fedha ambazo alikuwa amekwisha lipa haikuweko katika Kikao kile cha tarehe 19 Julai 2002.

(ii) Kuwepo Azimio kuhusu hoja hiyo katika kumbukumbu za kikao hicho siyo sahihi. Kwa hiyo, kumbukumbu hizo zimeghushiwa tu wala suala hilo halikujadiliwa!

(iii) Siyo utaratibu wa Kamati ya Hesabu za Serikali ya Bunge (*PAC*) kuandika kumbukumbu za vikao vyake. Kwa hiyo, kumbukumbu hizo katika hali hii ziliandikwa kwa ajili ya kazi maalum.

(iv) Kwa kuwa suala la deni la Mama Kitine lilikwischachukua muda mrefu sana na lilikwishaamuliwa, Kamati yangu haioni kulikuwa tena na umuhimu gani kiasi kwamba kumbukumbu zake ziandikwe haraka haraka na kusainiwa bila kufuata utaratibu!

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu uliotumika katika kujaribu kuondoa hoja ya deni la Serikali analodaiwa Mama Kitine na maamuzi ya kumrudishia fedha ambazo alikuwa amekwishalipa, Kamati yangu ilipokea na kujadili suala hilo kama ifuatavyo:-

(a) Katibu wa Kamati (*PAC*); Ndugu Mbise, alieleza kwamba Mheshimiwa Kabourou alimuagiza asambaze barua kutoka kwa Bibi Kitine na viambatanisho vyake kuhusiana na deni analodaiwa Serikalini.

(b) Mheshimiwa Dr. Kabourou anakubaliana na ushahidi huo na kueleza kuwa alifanya hivyo akiwa anataka ushauri kutoka kwa Wajumbe wengine. Hakuna ushahidi kuwa barua hiyo iliwasifika Wajumbe wengi, ila Ndugu Mbise alieleza kuwa alikwenda kuziweka kwenye “*pigeonholes*” zao, wakati Mheshimiwa Ndassa mwenyewe alisema kuwa barua hizo ziliwekwa mezani.

(c) Katibu Muhtasi wa Mheshimiwa Dr. Kabourou, Ndugu Rujina Mponzi, alithibitisha kuwa Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou, alimpatia barua hiyo na viambatanisho vyake ampe Katibu wa Kamati huyo; Ndugu Mbise azidurufu jambo lililoshindikana na kwa hiyo, ilibidi afanye yeze mwenyewe. Kwa mujibu wa Ndugu Mponzi, jambo hili lilifanyika tarehe 18 Aprili, 2002, lakini Ndugu Mbise na Mheshimiwa Kabourou walisema kuwa lilifanyika mnamo mwezi Julai, tarehe ambayo haikutajwa.

(d) Mheshimiwa Kabourou na Mheshimiwa Ndassa walikubali kuwa hoja ya deni la Mama Kitine ilikwisha jadiliwa na kutolewa maamuzi na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, haingeweza kufufuliwa tena na Kamati bila kupata kibali cha Mheshimiwa Spika.

(e) Mheshimiwa Kabourou alikubali kuwa hakumwarifu Mheshimiwa Spika juu ya barua inayosemekana iliandikwa na Mama Kitine.

(f) Mheshimiwa Kitine alieleza Kamati kuwa alimpelekeea Mheshimiwa Kabourou barua inayosemekana ilitoka kwa Mama Kitine na alieleza kuwa barua zote kutoka kwa Mama Kitine kuhusiana na deni lake zilikuwa zinawasilishwa aidha na ye ye mwenyewe au dreva wake. Alikiri kuwa amekwishamtumia Katibu Muhtasi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kuandika barua moja ambayo haikumbuki, lakini inayohusiana na deni la Mama Kitine.

(g) Mheshimiwa Dr. Kitine aliiambia Kamati kuwa siku ambayo haikumbuki na baada ya Mheshimiwa Kabourou kumwomba alimpelekeea barua ya Mama Kitine na viambatanisho vyake. Mheshimiwa Kabourou alikanusha!

(h) Katibu Muhtasi wa Mheshimiwa Kabourou, Ndugu Mponzi, alieleza kuwa mnamo tarehe 18 Aprili, 2002 Mheshimiwa Kitine alifika ofisini kwa Mheshimiwa Kabourou na akakaa na Mheshimiwa Kabourou kwa muda usiopungua dakika 45 na ni siku hiyo baadaye Mheshimiwa Kabourou alimpa barua ambazo alizitambua kutoka katika jalada la Mheshimiwa Kabourou ili ampe Ndugu Mbise azidurufu. Alisema hakuiona barua ya tarehe 20 Mei, 2002 ambayo inadaiwa kuwa ndiyo iliyo sambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati kuhusu hoja hii, Kamati yangu inaona kuwa kulikuwa na mpango dhahiri wa kuiwasilisha agenda ya deni la Mama Kitine upya mbele ya Kamati ya Hesabu za Serikali kwa mlango wa nyuma bila Spika kujua au kutumia mgongo wa *PAC* kufanya maamuzi mbadala yanayompendelea Bibi Kitine. Jambo ambalo lilikwishajadiliwa na kuamuliwa halingeweza kuletwa tena mbele ya Kamati bila idhini ya Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, Kanuni za Bunge zilivunjwa makusudi ili kutekeleza azma ya baadhi ya Waheshimiwa kuleta uamuzi mbadala juu ya deni la Mama Kitine.

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyo jitokeza ni kwamba, baada ya kusikiliza ushahidi wote na kufanya uchambuzi wa kina, Kamati yangu ilibaini yafuatayo:-

(a) Kamati inaona kuwa suala hili limeshughulikiwa kwa haraka sana kiasi cha kukiuka taratibu na Kanuni za Bunge katika utendaji wa Kamati za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni Na. 88(11), Kamati yoyote baada ya kukamilisha kazi inatakiwa kutoa taarifa kwa Spika ipelekwe Bungeni kwa uamuzi.

(b) Hata kama suala la Mama Kitine lingejadiliwa na Kamati ya Hesabu za Fedha za Serikali katika Kikao chake cha tarehe 19 Julai, 2002 ilibidi suala hilo liwasilishwe kwa Mheshimiwa Spika kabla hatua nyingine yoyote kuchukuliwa. Mheshimiwa Spika ndiye ambaye ana madaraka ya kuamua ni nini kifanyike.

(c) Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeridhika kwamba kulikuwa na mawasiliano ya karibu sana kati ya Mheshimiwa Dr. Kabourou na Mheshimiwa Dr. Kitine kuhusiana na suala la deni la Mama Kitine. Kamati inaamini kuwa kusingkuweko na mawasiliano hayo, hoja hii ya deni la Mama Kitine haingeibuliwa upya.

(d) Mheshimiwa Ndassa muda wote alikuwa anajua ni kitu gani kilichokuwa kinafanyika na alitumia nafasi yake kama Mbunge kuamuru watendaji wa Bunge kufanya ambayo dhahiri yalikuwa kinyume na Kanuni za Bunge.

(e) Kamati yangu imeona *Hansard* za kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali cha tarehe 6 Machi, 2002 na kubaini kuwa Mheshimiwa Dr. Kabourou tangu katika Kamati alikuwa anamuunga mkono Mama Kitine, kutokana na lugha aliyotumia katika *Hansard* hiyo inalingana na lugha iliyotumiwa katika muhsatari unaosemekana umetokana na Kikao cha tarehe 19 Julai, 2002.

(f) Mheshimiwa Kitine aliiambia Kamati yangu kuwa alipewa nakala ya barua ya msamaha wa deni la Mama Kitine iliyoandikwa na Katibu wa Bunge kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya wakati siyo yeye aliyesamehewa. Hivyo, ni dhahiri kuwa kulikuwa na mawasiliano ya karibu kati ya Mheshimiwa Dr. Kitine na waliohusika na mpango wote.

(g) Kamati yangu pia inaona kuwa haikuwa sahihi kwa Mheshimiwa Dr. Kitine kutangaza jambo la msamaha wa deni la mke wake katika mkutano wa Waandishi wa Habari kabla uamuzi haujafanywa na Bunge. Hata kama uamuzi wa Bunge ungetolewa, Bunge lenyewe ndilo lingekuwa chombo rasmi cha kutoa taarifa kwa vyombo husika, siyo yeye.

(h) Mara baada ya Mheshimiwa Kitine kuongea na Waandishi wa Habari, Mheshimiwa Dr. Kabourou alipohojwa na Waandishi wa Habari kuhusu maamuzi ya Kamati ya Hesabu za Serikali kumsamehe Mama Kitine, alisema kuwa Kamati yake ilikuwa na uwezo wa kurejea maamuzi yake na kuwa kilichofanyika kilikuwa sahihi. Hii inaonyesha kuwa Mheshimiwa Dr. Kabourou alikuwa anahuksika na maamuzi yote hayo, lakini aliamua jambo hilo litendeke wakati yeye hakuwa kwenye kit, alimsukumizia Mheshimiwa Richard Ndassa. Isingekuwa hivyo na huku akijua Kanuni za Bunge na kuwa hakuwa ameagiza suala hilo lijadiliwe, angelikanusha mara moja na kuchukua hatua wakati ~~mufaka~~. (*Kicheko*)

Kamati yangu inaona kuwa kikao alichoitisha baada ya muda wa Kamati kwisha na bila kibali cha Mheshimiwa Spika cha kuiongezea muda Kamati hiyo kilikuwa batili na alikuwa anataka kujikosha tu.

(i) Ndugu Mbise angestahili kuwa mwangalifu zaidi na kumshauri Katibu wa Bunge ipasavyo. Hata hivyo, Kamati yangu inazingatia muda wake katika kazi na ngazi yake katika utumishi wa Bunge na kuona kuwa inawezekana kuwa alizidiwa na shinikizo la Mheshimiwa Richard Ndassa. Alizidiwa, alizidiwa! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni ya Kamati, Kamati yangu inaridhika bila kuwepo na shaka yoyote kuwa makosa yafuatayo yalitendeka:-

Mheshimiwa Spika, kosa la kwanza ni kughushi muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Fedha za Serikali (*PAC*) cha tarehe 19 Julai, 2002.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeridhika kuwa Mheshimiwa Richard Ndassa, ndiye aliyekuwa *engine* ya kughushi muhtasari husika kwa sababu zifuatazo: -

(i) Ameshindwa kuithibitishia Kamati kuwa wale Wajumbe ambao wamekanusha kuhudhuria kikao cha siku hiyo kama walivyoorodheshwa walihudhuria.

(ii) Mbele ya Kamati, amejaribu kutoa maeleo ambayo hayaridhishi kuhusu Wajumbe kuandika majina ya wenzao wasiokuwepo.

(iii) Akiwa kama Mwenyekiti wa Kikao husika aliwajibika kutambua majina ya Wajumbe waliohudhuria. Kwa hiyo, kukaa kwake kimya kunaonyesha kuwa alikuwa na nia ya kuonyesha kuwa muhtasari huo uliridhiwa na Wajumbe wote.

(iv) Kwa ushahidi wa Katibu wa Kamati Ndugu Mbise na wa kwake mwenyewe (Mheshimiwa Ndassa), yeye alisimamia na kuelekeza uandishi wa muhtasari huo na pia aliuhariri kabla ya kuchapwa (*final version*).

(v) Pamoja na kwamba Ndugu Mbise pia alishiriki, Kamati inaona kwamba alishiriki bila kuwa na uwezo wa kukataa kwa sababu alikuwa anatii maelekezo ya Mwenyekiti wa Kamati yeye akiwa kama mtumishi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kosa la pili ni kosa la kula njama ya kubadilisha maamuzi ya Bunge (*Conspiracy*): -

(i) Kulikuwa na njama ya kubadilisha uamuzi ambao ulikwishatolewa na Bunge. Bunge kwa kushauriwa na Kamati ya *PAC* ilikwishardhia kuwa suala la deni la Bibi Kitine lipelekwe Mahakamani ikiwa angeshindwa kurejesha fedha alizopewa kwa ajili ya matibabu na baadaye kushindwa kuthibitisha zilivytumika, hasa baada ya kutoa risiti ambazo zilionekana ni za kughushi.

(ii) Kamati yangu iliambiwa kuwa risiti zilizotolewa na Mama Kitine zilikuwa ni za dawa za saratani na siyo za matibabu na zinahusu dawa nyingi kiasi cha kuonekana ziliagizwa kwa ajili ya duka zima la madawa na kama mgonjwa huyo angezitumia angefariki dunia. (*Kicheko*)

(iii) Kamati ilipokea ushahidi wa Ndugu Rujina Mponzi kuwa Mheshimiwa Dr. Kabourou alimpa barua kutoka kwa Bibi Kitine na viambatanisho vyake ili ampe Katibu Mbise azidurufu na kuzisambaza kwa Wajumbe wote wa Kamati. Jambo hili linaungwa mkono na wote.

Utata unaojitokeza ni kwamba, wakati Ndugu Rujina Mponzi anasema kazi hiyo ilifanyika tarehe 18 Aprili, 2002, wao wanasema ni mwezi Julai, 2002.

Kamati inashawishika kuamini ushahidi wa Ndugu Rujina kwa sababu zifuatazo: -

(a) Katibu Muhtasi huyo aliitwa na kuhojiwa mbele ya Kamati mara nne, mara ya tatu akiwa anatoa ushahidi mbele ya bosí wake Mheshimiwa Dr. Kabourou, lakini hakutetereka.

(b) Akitoa ushahidi (kweli yule mwanamke anajiamini sana) aliweza kukumbuka barua alizodurufu na akazielezea jinsi zilivyo tukiwa Dar es Salaam na tulieleza faili liletwe tukiwa na Mheshimiwa Dr. Kabourou, faili lililetwa na zile barua zilikuwemo. Kwa hiyo, alikuwa anasema ukweli.

(c) Kwa misingi hiyo Kamati inaridhika kwamba kazi ya kudurufu barua kwa ajili ya Kamati ya *PAC* ilifanyika tarehe 18 Aprili, 2002 na kwamba barua iliyodurufiwa na kusambazwa haipo kwenye faili la Dodoma kwa sababu nakala halisi (*original*) ilichukuliwa na Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, huku akiwa ameiambari Kamati yangu kuwa ni yeche kwa kudurufiwa na kudurufiwa na Ndugu Mponzi haifanani kabisa na saini nyingine zozote.

(iv) Kinachojitokeza katika hizo barua ni kwamba, barua tatu za Bibi Kitine za tarehe 20 Mei, 2002 (ambazo zinadaiwa hivyo) zenyé maudhui sawa, lakini zinatofautiana katika saini. Pia, saini ya Bibi Kitine iliyopo katika barua yake ya tarehe 6 Machi, 2002 na kudurufiwa na Ndugu Mponzi haifanani kabisa na saini nyingine zozote.

Kamati imeridhika kwamba saini za Bibi Kitine katika barua zilizoandikwa baada ya tarehe 16 Aprili, 2002 zimeghushiwa na hazikusainiwa na Bibi Kitine. Maeleo ni kwamba: -

(a) Katika barua tatu zinazofanana maudhui inayodaiwa kusambazwa na Wabunge ina mhuri wa *CONFIDENTIAL* juu na chini, wakati zile mbili zilizomo ndani ya faili binafsi la Dr. Kabourou, moja ina saini halisi (*original in blue ink*) na ni nene. Ile nyingine ni *photocopy* na ina saini nyembamba.

(b) Mheshimiwa Dr. Kitine aliiambia Kamati kwamba yeche na mkewe walifika ofisini kwa *RC Dodoma*, (ingawa alipoitwa mara ya pili alikana kwenda na mkewe kwenye ofisi ya *RC*) amchapie barua hiyo. Alisema yeche mwenyewe ndiye aliyeipeleka kwa Mheshimiwa Dr. Kabourou kwa vile wakati huo mkewe (Mama Saada Kitine) alikuwa amekwenda msibani huko Iringa (kama ndiyo, nani alisaini barua hiyo?)

(c) Mheshimiwa Dr. Kitine, katika mahojiano alikubali kwamba anamsaidia mkewe kwa mawazo na kuandika wakati fulani.

(d) Mashahidi waliofika mbele ya Kamati ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Kabourou mwenyewe walikubali kutofautiana kwa saini ndani ya barua zilizokuwepo mezani.

(v) Kwa kuwa barua hizo zimekutwa katika faili la Mheshimiwa Dr. Kabourou ofisini kwake na kwa kuwa hilo ni faili lake binafsi, Ka mati inashawishika kuamini kwamba Mheshimiwa Dr. Kabourou anafahamu kilichokuwa kinaendelea.

(vi) Kamati pia imearifiwa na Ndugu Rujina Mponzi na inaamini kuwa tarehe 18 Aprili, 2002, Mheshimiwa Dr. Kitine alifika ofisini kwa Mheshimiwa Dr. Kabourou na wakakaa kwa zaidi ya dakika 45 na alipotoka ndipo agizo la kudurufu barua lilipotolewa na Mheshimiwa Dr. Kabourou.

(vii) Mheshimiwa Dr. Kabourou amekubali ushahidi huu na akaongezea kwamba baada ya suala la msamaha wa deni la Bibi Kitine kuleta mjadala amewahi kukutana na Mheshimiwa Dr. Kitine mara mbili na Mheshimiwa Dr. Kitine akamtuliza kwa kumwambia: “Usijali ni mambo ya kawaida”. (*Kicheko*)

(viii) Mheshimiwa Spika, Katibu Ndugu Mbise alitoa ushahidi kuwa amewahi kumsikia Mheshimiwa Dr. Kabourou, akisema: “Dr. Kitine ametuanguusha!” Hii ilikuwa mara baada ya taarifa ya Mheshimiwa Bernard Membe aliyoitoa hapa Bungeni.

(ix) Aidha, umetolewa ushahidi na Mheshimiwa Ndassa kwamba Mheshimiwa Dr. Kabourou wakati anamwomba akaimu Uenyekiti wa kikao cha tarehe 19 Julai, 2002 alimtaka siku hiyo wajadili pia suala la deni la Mama Kitine na kumsamehe. “....ninakuomba mtakapojadili, mjadili pamoja na suala la Mama Kitine, ameshanilettea barua yake ikionyesha risiti alizotumia. Hivyo, mlitolee uamuzi wa kumsamehe. Unajua *issue* hii imeendeshwa kisiasa”.

Mheshimiwa Kitine akiwa mbele ya Kamati yangu, alitumia maneno hayo hayo kuwa suala la deni la mke wake ni la kisiasa tu! Maneno yake yanashabihiana na yale yaliyotumiwa na Mheshimiwa Kabourou katika *Hansard* ya tarehe 6 Machi, 2002 na katika kumbukumbu zilizoghushiwa na *Hansard* ya tarehe 31 Julai, 2002 wakati Mheshimiwa Dr. Kitine akichangia hapa Bungeni.

Ushahidi wote huu unaonyesha kwamba kulikuwa na njama baina ya Mheshimiwa Dr. Kabourou, Mheshimiwa Dr. Kitine na Mheshimiwa Richard Ndassa na mtekelezaji mkuu kwa bahati mbaya akawa Mheshimiwa Richard Ndassa, kwa kughushi muhtasari na kuupeleka kwa Katibu wa Bunge ili apeleke barua ya msamaha wa deni la Mama Kitine kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya. Jambo ambalo lilitendeka. Kuhusu ukiukaji wa Kanuni za Bunge, kwa kuzingatia ushahidi uliojadiliwa hapo juu, Kamati yangu inaona kuwa Waheshimiwa Wabunge wafuatao wanayo makosa kama ilivyoainishwa hapa chini:-

(a) Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou:-

(i) Kukubali kurejea upya jambo ambalo tayari lilikwishafungwa kwa kutolewa maamuzi na Bunge, bila kupata maelezo ya Spika.

(ii) Kutotafuta ushauri wa Spika kuhusiana na mawasiliano yaliyokuwa yanafanywa kwake moja kwa moja pasipo kufuata taratibu za kiofisi, yaani kupelekwa suala kwa Katibu bila idhini ya Spika.

(iii) Kutoa matamshi ya kuunga mkono maamuzi batili yanayodaiwa kufanywa na Kamati yake ya *PAC* na hadi pale mambo yamekwenda kwenye Vyombo vya Habari na ye ye mwenyewe akisema: “....kama tuna madara ka ya kutoa adhabu tunaweza pia kusamehe”.

(iv) Kula njama ya kubadili maamuzi halali ya Bunge kwa kujaribu kumfutia Mama Kitine deni analodaiwa na Serikali na kujaribu kumrejeshea fedha alizokwuwa amekwishalipa.

(b) Mheshimiwa Richard Ndassa:-

(i) Kula njama ya kusamehe deni la Mama Kitine analodaiwa na Serikali.

(ii) Kubadilisha maamuzi ya Bunge bila kufuata taratibu na Kanuni za Bunge.

(iii) Kughushi muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Fedha za Serikali cha tarehe 19 Julai, 2002.

(iv) Kushinikiza barua ya kusamehe deni la Mama Kitine iandikwe kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Afya kinyume na utaratibu na huku akifahamu kuwa hoja hiyo haijafikishwa Bungeni.

(c) Mheshimiwa Dr. Hassy H. B. Kitine:-

(i) Kutoa taarifa kwa Vyombo vyta Habari kuhusu maamuzi ya Kamati ya *PAC* akijua wazi kuwa taarifa yoyote ya Kamati za Bunge ni siri hadi itakapowasilishwa Bungeni.

(ii) Kula njama ya kufufua hoja ya deni na Mama Kitine kwa lengo la kulifuta na kumrejeshea fedha ambazo alikuwa amekwishazilipa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeshangaa kwamba ukiukwaji wote huu wa Kanuni za Bunge umeweza kufanywa na Wabunge wazoefu wa Shughuli za Bunge na hasa Chief Abdallah Fundikira ndiye aliyeshangaa kupita sisi wote, hakuamini yule mzee! Pia, kwamba jambo hili limefanyika bila kuwepo na ombi lolote la Mama Kitine la kufutiwa deni na kurejeshewa fedha ambazo alishalipa Serikalini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika barua aliyomwandikia Mwenyekiti wa *PAC* tarehe 20 Mei, 2002 Mama Kitine anasema, nankuu sehemu ya barua hiyo: "...Mwenyekiti, naomba kuwa jambo hili lisipelekwe Mahakamani kwa sababu kama nilivyojibu katika barua yangu kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kuwa nitajitahidi kadri ninavyoweza kumaliza deni hilo kabla ya mwisho wa mwaka 2000." Sasa kilichofanyika ni kitendo cha kukiuka maadili na ni udhalilishaji wa Bunge lako Tukufu. Kuhusu adhabu zilizopendekezwa, kabla ya kutaja adhabu gani zinastahili kutolewa kwa Waheshimiwa Wabunge wanaovunja sheria, kanuni na maadili, ni vyema kwa kifupi sana tukumbushane kwamba kila Bunge pote duniani lina kanuni zinazoliongoza. Mabunge mengine yana sheria zinazolinda haki na madaraka ya Bunge ili kusudi liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi bila kuingiliwa na chombo chochote. Suala hili lieleweke kwa Waheshimiwa Wabunge wote na wote waliomo humu ndani.

Mheshimiwa Spika, suala la haki za Bunge ni la kikatiba na sheria zimetungwa kwa ajili ya utekelezaji wake. Mfano, Sheria Na. 3 ya 1988 ya Bunge la Tanzania, inalinda haki hizo, katika Ibara ya 100 na Ibara ya 1 ya Katiba. Ibara ya 100 inatamka haki na ile nyingine inafafanua.

Mheshimiwa Spika, katika Katiba za nchi za Afrika Mashariki kwa mfano, ibara zifuatazo zinatoa haki kwa Mabunge yake:-

- (a) Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- (b) Ibara ya 57 ya Katiba ya Jamhuri ya Kenya.
- (c) Ibara ya 97 ya Katiba ya Jamhuri ya Uganda.

Mheshimiwa Spika: "*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Acts*" za nchi mbalimbali zina adhabu nyingi, zingine zina adhabu kali sana kama vile kumsimamisha Mbunge vikao, au kumsimamisha kazi ya Ubunge, au kumpeleka jela moja kwa moja kwa kipindi fulani na nyingine zinampa adhabu ya kufukuzwa kazi ya Ubunge moja kwa moja au faini. Mabunge ya Uingereza, Canada, Australia, Zambia, Alberta na kadhalika yana adhabu za namna hiyo. Nataka ieleteweke kuanzia leo na ni vizuri tuanje kusoma sasa. Katika kijitabu chako cha hivi karibuni: "*A handbook for New Members of Parliament*" na makala nyingine ambazo tumezipitia, kuna Mheshimiwa mmoja anaitwa Ron Brown wa Bunge la Uingereza - *The British House of Commons*, alipewa adhabu ya kutofika Bungeni kwa siku 20 kwa kosa la walichokiita "damaging the ace." (*Kicheko*)

Lakini katika Bunge hilo hilo, Mbunge mwininge Bwana Garry Allighan alibainika kusema uongo mbele ya Kamati kwa kusingizia Wabunge kwamba walipokea rushwa ili watoe siri za Kamati teule ya Chama chake cha Siasa kwenye Vyombo vyta Habari. Hatimaye iligundulika kwamba yeche (Allighan) ndiye aliye kuwa amepokea rushwa hiyo. (*Kicheko*)

Baada ya hayo: "*The leader for the House moved a motion that Mr. Allighan be suspended for six months without pay.*" But, another member moved an amendment proposing that Mr. Allighan be expelled from the House, instead of being suspended for only six months.

Hilo ni Bunge la Uingereza, achana na mambo haya. Hoja hiyo iliungwa mkono na Wabunge na Bwana Allighan alipoteza kiti cha Ubunge kwa kosa la kusema uongo akiwa Mbunge na kusingizia wenzake kwamba wamepokea rushwa na kumbe yeye ndiye mla rushwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza hapa ni kwamba, suala la Chama halikujitokeza hasa ikitiliwa maanani kwamba Mr. Allighan alikuwa Mbunge wa Chama Tawala kama CCM hapa, wakati huo *Labour Party* na *Labour Party* ndicho Chama kilichokuwa na Wabunge wengi, suala la Chama halikuungiwi, ni nidhamu ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Canada lilimfukuza Ubunge Bwana Fred Rose; Mbunge wa Montreal kwa kula njama za kutoa taarifa za nchi yake kwa nchi ya Uruusi. Tarehe 2 Mei, 1996 Waziri wa Hazina (wa Fedha) kama Mheshimiwa Mramba wa Bunge la *New South Wales - Australia* alisimamishwa kuhudhuria Bunge mpaka atakapoleta mezani nyaraka zilizokuwa zinatakiwa na *Legislative Council*. Alipogoma kutoka alivamiwa na *Serjeant-at-Arms* hadi nje ya Viwanja vya Bunge. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maana mkikaa kwenye giza mtakuwa mnashangaa vitu tarehe 30 Januari 1996 *very recently* Bunge la Zambia liliwahukumu hapa nataka rafiki zangu wajue kwenda jela moja kwa moja na kupigwa *fine* ya kwacha 1000. Waandishi wa Habari wawili, Ms. Lucy Sichome (na mimi mama yangu ni Nachone) Mr. Fred M'Membe wa Gazeti la *Post* kwa kuandika mambo ya uongo kuhusu shughuli za Bunge kwamba yangelifanya Bunge lionekane kuwa ni chombo cha ovyo mbele ya Umma. Moja kwa moja jela na faini hakuna kutoka Mahakamani. *It is provided in the constitution and in the written laws lazima twende na wakati. Mifano hiyo inatakiwa itufumbue macho kwamba adhabu kali zinaweza kutolewa na Bunge lako hili Tukufu.*

Pamoja na kwamba sheria Na. 3 ya Mwaka 1998, ipo dharau kwa Bunge hili *Contempt of Parliament* na kuzembea kwa wajibu wetu kama wawakilishi wa Umma vimekuwa vikionekana kutendeka hapa na pale. Sheria ya *Parliamentary Privileges and Powers* imekuweko tangu wakati wa *Legislative Council LEGCO* toka mwaka 1926. Lakini sheria hizi hazijawahi kutumika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Bunge lako tukufu lilishatoa adhabu moja tu. Ni ile iliyotolewa kwa aliyekuwa Mbunge wa Temeke Augustino L. Mrema la kutohudhuria Vikao vya Bunge kwa muda wa siku 40 kwa kosa la kutunga uongo mzito kiasi cha kuleta wasiwasi mionganoni mwa wananchi. Inakumbukwa hiyo Waheshimiwa Wabunge ndiyo hiyo peke yake sheria zipo.

Mheshimiwa Spika, inapendekeza adhabu hizi kwa mujibu wa Kanuni ya 60 (3) na Kanuni ya 61 pamoja na marejeo ya kesi mbalimbali siyo hii peke yake pamoja na marejeo ya kesi mbalimbali. Ofisini kwangu kuna kesi nyingi. Kesi mbalimbali za Mabunge mengine kwamba Bunge lazima liendelee kuwa chombo safi mbele ya Umma. Kwa maana ndiyo sauti yao. (*Makofi*)

Kwa makosa ya kukiuka Kanuni za Bunge, kughushi na kula njama za kufuta deni la Bibi Kitine hivyo kujaribu kuikosesha Serikali mapato makosa ambayo ni dhahiri yamelidhalilisha Bunge. Kamati inapendekeza kuwa wahusika yaani Mheshimiwa Richard Ndassa, (Mbunge), Mheshimiwa Dr. Aman W. Kabourou, (Mbunge) na Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, (Mbunge) wapewe adhabu ya kusimamishwa kazi ya Ubunge kwa muda wa miezi sita kuanzia tarehe ya Azimio la Bunge hili, ili iwe fundisho kwa sisi wengine wote. Kwa kweli kwa hili tulikuwa tunataka waende mahakamani lakini tumewapa adhabu hii ndogo kwa wengine ni mara ya kwanza wengine ni mara ya pili. Tulitaka waende Mahakamani huko wangepambana na sheria ngumu zaidi.

La pili, kwa upande wa Katibu wa Kamati ya *PAC*, Ndugu Elisa Mbise, Kamati inapendekeza kuwa Ofisi ya Bunge impe karipio kali kuwa awe mwangalifu katika kazi yake na anapoona anashinikizwa kufanya jambo lolote kinyume na taratibu na Kanuni za Bunge atoe taarifa mara moja kwa wakuu wake wa kazi kwa ajili ya ushauri na maelekezo. Hatua kali zitachukuliwa dhidi yake endapo atarudia makosa hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya kamati yangu naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, naafiki.
(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu hoja za Kamati hazina Msemaji wa Serikali wala wa Upinzani. Kwa hiyo, tunaingia moja kwa moja kwenye mjadala na nimeshapata maombi manane (8) kwa ajili ya kuchangia hoja hizi mbili.

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika suala moja zito kabisa ambalo limetokea katika Bunge letu kuchangia lakini *Inshallah* Mwenyekiti Mungu atatupeleka.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimeshuhudia taarifa zote mbili zilizowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati na kwa kweli ni taarifa nzito sana. Kweli sina budi kuwapa pole wote waliohusika na janga hili kubwa. Lakini taarifa zote mbili ni nzito kwa kweli mimi nimehuzuni sana na nasema haya siyo kama nabahatisha, nilibahatika kuhudhuria mafunzo katika Jeshi la Polisi na Namba yangu ilikuwa C. 9073 na nilikuwa niko makini sana kwenye masuala ya upelelezi. Kuna matukio unaweza kuthibitisha kama ni kosa la jinai kutoptaka na uzito wa lile tukio liliyyotokea, eneo lilitokea na mengine kwa kuona, kwa kusoma na kwa kusikia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchango wangu nitakaotoa sitaki nibahatishe, nataka nizungumze kwa uwazi kwa nia safi kwa faida ya Taifa letu hili la Tanzania. Pia nimeyasikia maamuzi yaliyotolewa. Lakini kabla sijaanza kuchangia nataka nimnukuu Baba wa Taifa kidogo katika hotuba zake ambazo huwa namsikiliza.

Moja ya Hotuba ya Baba wa Taifa ilisema kwamba hatuwezi kuchezza Katiba, Katiba ambayo inaongozana na sheria, Katiba ndiyo sheria ya msingi, sheria mama ambayo ni ya kuendesha mambo yote katika nchi. Kwa kweli masuala yote haya yanagusa uzito wa Bunge letu Tukufu, uzito wa Taifa letu, uzito wa wananchi wetu. Kwa hiyo, nashukuru kwamba pamoja na maelezo yaliyotolewa, pamoja na adhabu zilizotolewa na maombi yaliyokuwepo kwa kweli mimi nataka niwape pole walioyafikisha na niwatake Waheshimiwa Wabunge wayaone haya. Kuna masuala mengine jamani tusiingie tu ovyo ovyo ni masuala mazito kabisa. Ni masuala yanaweza kumwangamiza ~~mu~~ kwa kiwango kikubwa na kumwondolea utu wake. Suala la sheria ni suala pana sana.

Mheshimiwa Spika, mimi naungana na taarifa aliyowasilisha Mwenyekiti wa Kamati moja kwa moja nikiwa kama ni Mbunge wa Bunge hili na nikiwa ni kiongozi mmoja katika Taifa hili na hasa nikiangalia wajumbe walioshiriki katika kujadili matatizo haya ambayo mimi nitanukuu watatu tu, tukisema kama ni masuala ya Upinzani alikuwepo ndugu yetu Benedicto Mutungirehi. Lakini kuna watu wazito walikuwepo ambaa walikuwa wanasiliza na hata alipounga mkono Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mzee wetu Mheshimiwa Chief Abdallah Fundikira kwa *age* zao kwa elimu zao, kwenye masuala ya sheria kwa kweli haya masuala yalikuwa ni mazito. Kwa hiyo, kubwa tuwape pole wenzetu na hatua hizi ambazo zimewasilishwa. Nataka nirudie kuwataka Waheshimiwa Wabunge, jamani kuna mambo mengine tunatakiwa tuwe waangalifu sana.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye suala la Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, kuna masuala ambayo yamezungumziwa hapa kwamba hata alipotakiwa kuthibitisha kwamba mfanyabiashara akitaka mambo yake yamnyokee sharti aingie CCM, ili ufanye biashara usiguswe na *TRA* ni lazima uingie CCM.

Mheshimiwa Spika, sisi tukija hapa mimi nataka tujione kama ni viongozi. Hapa nafikiri tunakosea vingi, tunakuwa tunajigawa sehemu mbili. Maendeleo yote ya nchi yanategemea watu. Sisi wote tuko katika jamii ya watu na tukija kwenye masuala ya kulumbana hatufiki, tunajenga taifa la kuleta maendeleo makubwa. Taifa haliezezzi kuendelea bila kuwa na umoja. Maeneo ambayo yanagawa uzito wa Taifa ni umoja yakichanganya wasomi wetu na watalaa walipo katika nchi. Sasa tutaleta mambo kama haya ya kubishana hatufiki Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nazungumza kwa huzuni na nikakaa nikijiuliza janga kama hili lingenikuta kama mimi Mjaka ninglikuwa wapi? Nashukuru kwamba haya maamuzi yametolewa kwamba yasiende Mahakamani, nashukuru sana Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ya *fogging* ni kosa la jinai tena mazito kama haya ambayo yanagusa jamii, fedha ya Serikali. Kwa hiyo, na nikiangalia kwamba kuna maeneo alitakiwa atoe ushahidi alishindwa kutoa ambayo kuna mambo kama manne aliyoyathibitisha. Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo naungana nayo na kwa sababu kuna watu pale walioshiriki katika kamati na maamuzi yaliyotolewa yamewasilishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini ninanukuu ukurasa wa 4 Kamati imesema: "Bunge lako ni chombo kitukufu kamwe lisigeuzwe kama *club* ya masuala ya kisiasa ndipo nilisema jamani hiki ni chombo muhimu. Tushukuru kwamba Kamati imeweka masuala haya kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii kama itatolewa kwa uwazi kwa watu wetu mimi nadhani niseme Bunge ni la kujiuzulu siyo siri kwa sababu ni Kamati nzito ya Bunge iliyojadili. Pamoja na kwamba tushukuru wenzetu watatu waliobeba mzigo huu, wengine wanasesma msalaba wametuokoa. Lakini ni suala zito na siwezi nikasema ni kashfa ya aina gani ambayo imelikuta Bunge letu. Kwa hiyo, nataka niungane na Kamati juu ya maamuzi yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika taarifa ambayo imemgusa Mheshimiwa Richard Ndassa na juu ya hoja ya Mama Saada Kitine kwa kweli inasikitisha na nataka nirudie kwamba kwa sababu kuna watu wazito hapa ambao walishiriki katika Kamati hii na mtu mkubwa sana wa nidhamu ambaye lazima wote tumheshimu ni Mheshimiwa Chief Abdallah Fundikira kwa *age* yake asingekubali kubeba jukumu kubwa kama walitufanya haki nchi yetu kuipigania huko nyuma mpaka hapa tulipo wasingeweza kuwatumbukiza watu katika janga hili kubwa. Kama Mheshimiwa Chief Abdallah Fundikira alisikitika na mimi nasikitika sana juu ya janga kama hili.

Mheshimiwa Spika, nanukuu katika ukurasa wa pili iko orodha ya wanakamati ambao walihudhuria, imewahusisha wazee wetu hawa. Kwa sababu haya masuala yasije kuja baadaye tukalumbana, kwamb a labda Bunge au wengine waliochangia, wamechangia kwa sababu ya kujipendekeza, ni nia moja ya kulisafisha Bunge letu, kuisafisha nchi yetu kwa nia safi.

Mheshimiwa Spika, lakini nanukuu ukurasa wa 28 imesema hapa "..... Mwenyekiti, naomba kuwa jambo hili lisipelekwe Mahakamani kwa sababu kama nilivyojibu katika barua yangu kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, kuwa nitajitahidi kadri ninavyoweza kumaliza kulipa deni hilo kabla ya mwisho wa 2003".

Mheshimiwa Spika, hili ombi tusilipuuze kama imeshapita hukumu nataka tulichukue hili ombi la huyu mwananchi au mwanadamu mwenzetu. Kwa sababu suala la kisheria wanaweza tu wakatoka watu wakawashawishi hawa wenzetu ambao wamepata adhabu hii na wakatafuta vyombo vingine na tukisema tukimbilie Mahakamani likaja likazunguka likaingia katika mgogoro wa Kiserikali tujaribu kuangalia wapate washauri wazuri, wajaribu kutulia na tuangalie miezi sita siyo mingi, kuna kipindi lazima binadamu utakutana nacho kama hicho.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nirudi nyuma katika ukurasa wa 29 inasema suala la haki ya Bunge ni la Kikatiba na sheria zimefungwa kwa ajili ya utekelezaji wake mfano sheria Namba 3 ya mwaka 1988 ya Bunge la Tanzania hapa ndipo iliponipa kukubaliana na taarifa hizi mbili. Kama nilivyojosema mwanzo nilivyonmukuu Baba wa Taifa sheria ndiyo msingi, ndiyo maana Katiba imegusa, kwa sababu Katiba imelipa uwezo Bunge kwa mujibu wa sheria zilizopo zinazoendesha. Kwa hiyo, nawataka Waheshimiwa Wabunge, hilo ni somo kwetu kwa taifa letu kwa wananchi na siyo jambo la kufanya masihara. Tukitoka hapa tujiulize na tuwe na wenzetu kwa muda wote mimi ni mmoja kama jambo hili limemgusa Mheshimiwa Richard Ndassa limenihuzunisha sana. Nina uhusiano naye mkubwa sana.

Nataka niseme kwamba ni Mbunge ambaye nashukuru kwa ushirikiano mkubwa niliyopata mwaka 2000 nilipoingia hapa Bungeni na wenzangu na laiti kama ningelizwa mwanzo ningesema muda ya miezi sita ni mingi sana. Tujaribu kumwekea miezi fulani ili mwenzetu tuungane naye pamoja, tunamjua ukweli wake na juhudhi zake. Lakini wakati adhabu imeshapita na imeletwa mbele ya Bunge

hatuna la kufanya. Nazungumza ndani ya nafsi kabisa na kama kuna kipengele ambacho hakitaki malumbano mimi naliomba Bunge, Serikali na Wananchi wa Tanzania juu ya hili kwa sababu haya mambo toka nyuma na kwa bahati mwenzetu AmaniKabourou alithubutu kusema kwamba jamani mwenzetu ametuponza jamani ni kilio peke yake. Hawa ni Waheshimiwa Wabunge. Vyombo vitatu muhimu katika nchi ni Bunge, Mahakama na Serikali. Dhahiri tuzungumzeje tusaidiane kwa hili. Kwa hiyo, kama itawezekana *serious* kabisa, Mheshimiwa Richard Ndassa, nimekuwa naye muda mrefu sana, ni mkweli sana. Lakini kuna mitego na mtihani binadamu wote hawawezi kuepukana nayo.

Ikiwa Serikali inaweza ikatazama ombi hili juu ya wenzetu kwa sababu ni watu muhimu. Tangu 2000 Novemba mpaka leo wametoa michango mikubwa hapa Bungeni. Mheshimiwa Richard Ndassa, wakati wote wa Bunge tunakuwa naye, ni mzungumzaji mzuri sana yupo pamoja na watu muda mwingi sana. Lakinikwa mtihani huu hatuna la kufanya. Kama kuna uwezekano tunaomba radhi juu ya Serikali, juu ya Bunge, juu ya Mahakama kama suala litapelekwa huko, juu ya wananchi wetu wa Tanzania. Lengo ni kuunganisha wananchi wetu wa Tanzania siyo kwa kubahatisha. Kama tutakuwa tunapungua kiasi hiki kwa kweli itakuwa ni kasoro kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nakubaliana na taarifa hizi lakini pia nataka nitoe *special request* juu ya tatizo hili kama itawezekana juu ya kuffikiria wenzetu ipunguzwe adhabu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kusaidia mjadala tu kwamba hoja iliyoko kwenye *Order Paper* ni kwamba Bunge lipokee na kukubali mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa. Sasa tukijielekeza kwenye mapendekezo tutarahisisha kazi ya uamuzi baadaye. Samahani sikuwataja wanaofuata baada ya hapo ili wajiandae lakini alipangwa kufuata baada ya Mheshimiwa Omar Mjaka Ali ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na atafuatiwa na Mheshimiwa William Shellukindo.

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuchangia hizi hoja mbili zilizoko mbele yetu. Nianze kwa kuwapongeza Mwenyekiti na Kamati yake kwa kazi nzuri sana walifofanya na ya kina sana.

Mheshimiwa Spika, labda nianze na hili ambalo ni la Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo. Kuhusu hoja ya Mheshimiwa Ndesamburo mimi nisingelipenda kuichangia sana kwa sababu moja kubwa. Taarifa niliyonayo ni kwamba baada ya matukio yaliyotokea Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo alifungua kesi Mahakamani na ninaambiwa kwamba kesi hiyo, iliamuliwa na Mahakama Kuu na sasa inakwenda Rufaa. Mimi ningependa kuheshimu zile taratibu na Kanuni zetu kwamba jambo likiwa mahakamani basi tusilzungumzie na sababu zilizotolewa nafikiri zimeelezwu na kwenye magazeti wametaja pia hukumu ya Mahakama imetutaja pia tulikosea. Kwa hiyo, nisingependa kuongelea hili la Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo. Lakini kuhusu hii hoja ya pili, mimi naungana kwanza na Mwenyekiti wa Kamati, kwamba suala hili lisiwe na vyama na lisiwe la kiitikadi. Mimi ninaungana na Mheshimiwa aliyetajwa alishangaa *Chief* na kushangaa mtiririko mzima wa kitu kilichoelezwa hapa na kama kweli yalitokea yalivyoolezwu hapa basi mimi nafikiri tuna tatizo zito zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kamati imefanya kazi ya kina sana na kwa hili tofauti na lile lingine nafikiri hapa *procedure* karibu zote zimefuatwa. Kwa hiyo, mimi naomba nipokee hii taarifa kwamba najielekeza kuipokea na kuikubali hiyo taarifa ilivyo. (*Makofî*)

La kwanza ambalo ninaliona ni tatizo la taratibu zilivyokiukwa. Taratibu za kawaida za Bunge na Kanuni za Bunge zilivyokiukwa nimezielewa japo ninaweza kusema kwamba taratibu hizi zinaweza kuwa *mitigated* ni kweli Spika, hakupewa taarifa nakadhalika. Lakini hizi ningeliona kwamba siyo *serious* sana kwa sababu kanuni zetu zinaruhusu Kamati iweze kujadili jambo lolote, aidha kwa kuombwa na Spika au kwa zenyewe pia kuanzisha jambo. Kwa hiyo, kwa zenyewe kuanzisha ningeliona kwamba labda walikuwa na sababu ya kuanzisha jambo hata kulifufua, labda wangeweza kulifufua. Lakini baada ya pale taratibu zingine zingelifuatwa. Hilo halinipi taabu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini linalonipa taabu mimi, halinipi pia taabu suala la Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, kufuutilia masuala ya mke wake. Mimi nafikiri sisi sote tunafahamu kama kuna mwenzako kumpelekea barua, kupeleka ujumbe, halinipi taabu, linaweza kuwa ni ushahidi wa mazingira wa kitu kilichotokea. Lakini halinipi sana shida.

Mheshimiwa Spika, lakini tunapofika mahali kwamba kwanza kuna tatizo la kughushi mimi hili linanipa shida. Tunapofika mahali kama kuna ushahidi wa kughushi na unagushiwa na Waheshimiwa ambao wanatakiwa kulinda sheria, hili linanipa mimi shida na nimesema hapa ninaweka suala la itikadi pembeni na Mheshimiwa Aman Kabourou ni ndugu yangu ni rafiki yangu, kiongozi wangu.

Kwa hiyo, ninapoliongea hili siongei kwa sura yoyote, ninaongelea suala la uzito wa tatizo na sisi Wabunge tunapaswa kukemea popote pale inapokuwa na bila kujali itikadi. If it is true kwamba kuna suala ambalo limehusisha jambo ambalo bahati mbaya Kamati haikufanya ilitegemea ilifanye na labda ningetaka suala hilo bado hata kabla ya kufungwa nilifanye unapofikia suala zito kama la kughushi, nchi yetu ina taratibu ya *ku-prove* kwa kutumia *Identification Bureau (IB)*. Unapofikia mahali mtu unayemtuhumu ni Mbunge ambaye ni kiongozi mzito na hujaifikia hatua hiyo kidogo ni *weakness* kwa upande wa kwetu wa Kamati. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningeliomba kwamba taratibu hizo kama kuna suala la kughushi, isiwe kwa Mheshimiwa Richard Ndassa, iwe kwa Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, anatuhumiwa kugushi saini za Mama Saada Kitine, haijatajwa ni Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine au ni Dr. Amani Kabourou au ni nani lakiniimeachwa wazi, mimi nilifikiri pale kulikuwa na suala zito la kuthibitisha ni nani aliyeghushi zile saini ambazo zinasemekana zinatofautiana, hili limeachwa hewani. Hapo nilitegemea kabisa Kamati yetu ingelipeleka kwa vile vyombo na vyombo viro na hatukuwa na sababu ya kuharakisha suala hili kulitolea taarifa kabla ya kupata ufanuzi. (*Makofi*)

Lakini inanipa tatizo kwamba tayari kuna hisia ya kwamba kuna kughushi hilo kwa peke yake mimi imenipa shida na unapofikia mahali kwamba mwelekeo mzima ni wa kutoa taarifa ambayo unaghushi na kwanza tulianza kusikia hisia kwamba zilisainiwa kwenye kantini. Baadaye tukasikia kwamba imesainiwa bila Kamati kukaa. Baadaye tukasikia kwamba Kamati ya Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou, nayo imekaa nje ya muda na nafikiri ni Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo kwa taarifa nilizosoma kwenye magazeti alisisitiza Mheshimiwa Spika, atuambie Kamati ya Dr. Amani Kabourou ilikuwa na uhalali gani?

Mheshimiwa Spika, kwa wakati fulani nafikiri kwa nia njema ulisema kwamba sijapata ushahidi. Lakini alipothibitisha tena kwamba ni saa 7.30 wakati uhai wa muda umeisha, haya ni mambo ambayo kwa kawaida huwa hatuwi makini kuzingatia. Kwisha kwa uhai wa muda wa Kamati, inaweza kuwa ni suala la kubatilisha jambo zima. Lakini kama hauna nia njema nyingine basi ile nia uliyokuwa nayo inaweza kuvunjika. Kwa hiyo, mimi nilifikiri hili ni suala zito na kwa kweli lilihitaji tulifanyie kazi.

La tatu ambalo ningependa kulisitisiza kamati imependekeza adhabu za kutolewa. Mheshimiwa Richard Ndassa rafiki yangu, Mheshimiwa Amani Kabourou rafiki yangu, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine rafiki yangu. Lakini kwenye haki na taratibu mimi naomba urafiki niuweke kwanza pembeni na naomba sana tusameheane katika hilo. Mimi ninashindwa kuelewa kwamba Kamati pamoja na kwamba hajamaliza kazi yake inatoa pendekeso kwenye Bunge, kwamba tumalizie kwa kuwatoa nje kwa miezi. Mimi hili silioni kama ni sahihi. Suala la kughushi ni kosa la jinai linapaswa kupelekwa panapostahili. Huwezi kuhukumu na Bunge likachukua jukumu la kuchukua kosa la jinai likaihalalisha na likaitolea maamuzi yenywewe.

Hapa mimi nafikiri tutakuwa hatujatoa mfano mzuri kwa taifa hili kwamba kosa linalotakiwa lipelekwe mahali, linapelekwa mahali linapostahili. Sasa ninakubali na ninaona hapa ndiyo uzito kwamba Kamati ya Mheshimiwa Eliachim Simpara, haijakamilisha kazi yake hata kupeleka Mahakamani inaweza kuwa ni ngumu kwa sababu hatujapeleka *Identification Bureau*. Lakini vizuri tukaifanyia kazi, tukatambua kwamba kweli kuna kosa hili la kughushi na aliyeghushi ni fulani, fulani na kwa sababu hiyo anastahili siyo tu adhabu ya kinidhamu ambayo Bunge, ndiyo yenyе mamlaka ya sasa hivi. Kanuni zetu zinatoa adhabu za kinidhamu lakini adhabu za kijinai kwa kweli mimi nafikiri ni nje ya mamlaka ya Bunge na inatakiwa kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria zilizoko ndani ya nchi yetu na Katiba yetu inaruhusu

jambo hilo. Kwa msingi huo mimi ninasisitiza kabisa kwamba pendekezo la Kamati, sawa kwa makosa ya nidhamu, lakini pendekezo la Kamati haifiki mahali pake inapofikia suala la kijinai.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningelipenda kulisema ni tatizo zima la jinsi *process* hii ilivyokwenda. *Process* hii sina hakika kabisa kama Mama Kitine pia naye anahusishwa hapa. Nimeona Mama Kitine hakuhusishwa, hakuitwa, hakuulizwa ina *weaken* kwa kiasi fulani kazi iliyofanywa na Kamati yetu.

Kamati ilitakiwa iwe *thorough* zaidi kwa jambo zito kama hili kwa kumpata pia Mama Kitine. Huwezi kutamka Mama Kitine hapa kwamba hakuwa na kosa la saratani na unafikia mahali kusema kwamba angekunywa zile dawa angekufa, lakini mwenyewe hujamhoji. Mimi nafikiri hapa tunajenga *premises* ambazo zinaweza kuwa ni za hatari huko mbele.

Kamati ifanye kazi *thorough*, ihakikishe kama inatenda haki, itende haki kwa kila mtu hata akiwa na makosa ana haki pia ya kusikilizwa kama mwanadamu na Bunge linapofuata taratibu zake kwa *quasi judicial* ifuate taratibu za *quasi judicial* ambayo ni mtu apate *natural justice* na kusikilizwa na aweze kuamuliwa.

Lakini huwezi kumwandika kwenye *document* nzito kama hii na kusema huyu angelikuwa amekufa. Hapa ni kosa zito na ambayo kamati haitakiwa na hairuhusiwi kuifanya na tukiruhusu makosa ya namna hii nafikiri tunafanya makosa makubwa sana.

Nilitegemea kama Kamati inafikia hatua hiyo, ingefika mahali Mama Kitine angepelekwa hata *Ocean Road* akapimwa kama saratani *at any one stage* ilikuwepo au haikuwepo. Hapa tungelikuwa na sababu nzito ya kusema Kamati yetu kweli hapa imefanya.

Sasa haya ni makosa ambayo tunawenza kusema *ina mitigate*, *ina-weaken* mapendeleko zaliyotolewa na Kamati yetu na taratibu zile za kawaida pia zinapunguzwa na sisi kama Wabunge saa nyingine hatujui hizo *procedure* tunapokea kamati kwa sababu tunaamini Kamati ilipitia. Lakini ukipitia watu waliohojiwa mimi sikuona jina la Mama Kitine kama amehojoji au vipi. Kwa hiyo, nilifikiri kwamba nina sababu nzito kabisa ya kuweka *reservation* kwamba Kamati yetu imefanya kazi nzuri lakini Kamati yetu ina *weakness* pia katika maeneo haya hasa kwa *include* mtu ambaye hujamshirikisha, hujamhoji halafu unamfanya *conclusion* ndani ya taarifa na taarifa hiyo inam-*destroy* na ye ye katika *repetition* yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ningependa kwa kumalizia kwamba ninapenda kutoa masikitiko yangu kwamba suala hili ni zito na ni zito ni la kijinai, lina sura ya nidhamu ambayo sisi tunawenza kutolea maamuzi lakini lina sura ambayo lazima liende mbele zaidi.

Kwa hiyo, mimi ningependekeza kwamba mimi siridhiki kama taarifa ilivyo, taarifa iende mbele zaidi na kasoro zilizopo zirekebishwe kwa kuweza kuwahuishwa wote wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hapo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijakuita Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, amegusia jambo la Kanuni kwamba kama kuna kunu jambo liko mahakamani wakati ule haliwezi kuzungumzwa Bungeni. Sasa mimi nitamwomba Mwanasheria Mkuu ajiandae kututolea ufanuzi. Mimi sijui kama kuna jambo liliko Mahakamani sasa kuhusu taarifa ya Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo.

Wote tumesikia tu kwenye vyombo vyoma habari, kwamba Mwanasheria wake anakusudia kuchukua taratibu za kukata rufaa, hatujaambowiwa kwamba ameshakata rufaa na hasa anakata rufaa juu ya nini. Tulichosoma katika magazeti ni kwamba anakata rufaa *on a point of law* siyo kwa tuhuma za Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo *on point of law*. Jaji wa Mahakama Kuu, alisema mahakama haina uwezo wa kushughulikia jambo hili kwa sababu linahusu taratibu za Bunge. (*Makofi*)

Tulivyosoma ni kwamba ye ye anakata rufaa kwa *point* hiyo ni kweli Mahakama haina uwezo wa kushughulikia si dhidi ya hukumu iliyotolewa ndivyo tulivyopata kwenye vyombo nya habari.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaomba Mwanasheria Mkuu ukishirikiana na wanasheria wenzako waliomo humu Bungeni akina Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro na wenzako baadaye mtupatia ufanuzi wa jambo hilo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni yangu kuhusu taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu tuhuma zilizozuka hapa Bungeni zilizotokana na Mheshimiwa Ndesamburo. Kwanza napenda kuipongeza sana Kamati hii kwa kufanya kazi kwa ufanisi, uadilifu, bila uwoga na bila upendeleo. (*Makofi*)

Kwa kweli wamelifanya Bunge kazi nzuri sana. Ni kazi ngumu kushughulikia wenzako ambao wote mpo hapa. Kwa njia moja, ni jambo zito sana. Lakini wao ni viongozi na Bunge, ni chombo cha Taifa, inabidi lifanye mambo ya kuonyesha mfano kwamba kama mtu amefanya kinyume na taratibu ashughulikiwe na wenzake, maana mnatazama Kanuni, sheria na taratibu, ndio kitu cha msingi. Kama yanatoka nje ni tofauti.

Mheshimiwa Spika, napenda sana nimponeze Mwenyekiti Simpassa. Mimi huwa namtania namwita kwenye mabano Mwenyekiti Kalikali. Lakini kinachofanyika kwenye Kamati yake ni kuwa *fair and firm*. Hizo tumeiona. Hicho ndicho kitu cha msingi kabisa. Pale mahali ambapo limetendeka kosa, basi tuwe *firm*, pale ambapo tunaona ni maneno tu hakuna kitu cha msingi, basi tuwe fair katika hali hiyo. Kwa hiyo haya nadhani ni mambo mazuri sana na nampongeza kwa jinsi anavyoendesha vikao vyake na kufikia mpaka uamuza ambao hakuna anayeupinga, tunakubaliana wote. Hii nadhani ni demokrasia ya haki katika Kamati ya Bunge kushughulikia matatizo yanayotokea Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda sisi wenye Wabunge tukumbushane kwamba tuna kanuni hizi, tumezitunga. Tuzisome, tuzielewe ili baadaye tusionekane sisi wenye kwa Kanuni zetu, tunafanya mambo halafu baadaye tunakuja kushtukia kumbe kuna Kanuni ya 50 inasema usifanye haya; hata wananchi watatucheka, kwamba mna Kanuni, kwa nini mmefanya hivi? Hizo wengine wanazo hizo!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na sisi wengine tunaosema hapa, tuseme lakini anayosema huyu mbona yanapingana na Kanuni walizotunga mle ndani? Sasa ni vizuri sisi wenye tufike mahali kwa kweli tuonekane ni chombo ambacho kinazingatia Kanuni ambazo tumeziweka, tusije tukafika wakati kama unavyotukumbusha mara kwa mara tukageuze Bunge hili kuwa ni jukwaa la Taifa la malumbano na porojo za kisiasa. Tumeletwa hapa na wananchi tutetee maendeleo yao. Ni vizuri tutumie muda huu vizuri katika kuangalia namna gani tuongoze katika maendeleo yao, ndio suala la msingi. Kwanza wengine wanashangaa kama tunapoteza wakati, tunazungumza mambo ya malumbano tu ya kisiasa ambayo kuna majukwaa kule, nao wanangojea wasikilize kule na watuulize maswali sio hapa ambapo wanataka wasikie matatizo yao ya maji yamezungumziwaje, ile barabara yao imezungumziwaje, lakini leo tunatumia muda wa Bunge kwa hizi hoja ambazo kama tungezingatia Kanuni hizi wala zisingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja ambalo nilitaka kukuuliza, nikasema hapa kwenye Bunge, Mbunge ukimsingizia mwenzio kuna Kanuni. Je, Mbunge akitoka akienda kwenye Jimbo la Mbunge mwenzake na akamsingizia. Je, kuna Kanuni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kanuni zetu ziko kimya. Lakini nimelitazama kwa upande mwingine, nimewahurumia sana wenzangu ambao wengine walikuwa kwenye Kamati za Bunge, Wabunge wengine wako kule wanavuruga shughuli zao za maendeleo. Ndiyo! (*Makofi*)

Lakini hao nawashauri kwamba kuna sheria ya uchaguzi. Zipo sheria za uchaguzi nadhani hata *Attorney General* utanisaidia ya mwaka 1985, inaeleza wakati gani wa kufanya kampeni. Sasa Wabunge wenzangu watu kama wamevunja sheria hiyo, wachukulieni hatua kwenye Majimbo yenu. Mimi wakija kwangu wakaenda kinyume cha sheria hiyo nitawapeleka wanapostahili. Sasa nashangaa, tuiswanyamazie, wanavuruga fedha zenu za maendeleo. Ukienda kwenye Jimbo ukasema Mbunge hakufanya hivi, maana yake nini? Si kampeni ya uchaguzi hiyo? Kwa hiyo wamevunja sheria. Tumieni sheria, tutakwenda vizuri. Mimi huo ndio ushauri wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kabisa mapendekezo ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, pamoja na adhabu iliyotoa. Tusioneane aibu. Wakati mwingine ni njia nzuri ya kuonyana, pengine utaweza kufanya makubwa zaidi ambayo yatakuwa na adhabu kubwa zaidi. Nakumbuka Mwalimu wangu mmoja wa *Middle School*, kama mwanafunzi amekosea, anaitisha bendi na wanafunzi wote mnakuwa pale halafu unapigwa muziki unaitwa: "Maisha Matamu Lakini Mafupi." Hujapewa adhabu, unasikiliza muziki ule, ukimaliza ndio unapewa adhabu: "Maisha Matamu Lakini Mafupi." (*Kicheko*)

Mwalimu wangu huyo alitoa tafsiri ya adhabu kwa Kiingereza akasema na anaitoa kabla hujaadhibiwa. Anasema: "*A punishment if properly perceived and administered, should work as a deterrent deterrent*". Yaani hiyo ni ya kumbukumbu kwamba siku moja mwenzetu alikosea alifanywa hivi, kwa hiyo mimi siwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, tuyazingatie hayo. Ndio maana kulikuwa na *quotation* kwenye taarifa zile za adhabu ambazo Bunge tumewahi kuzitoa hapa kutoka Mabunge mengine kwa maana ya kuturudi sisi Wabunge ili tuzingatie kanuni tusiingie kwenye mambo ambayo yanatupotzeza muda wetu wa kuchangia maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu taarifa yao ya kwanza. Ahsante sana. (*Makofit*)

SPIKA: Ahsante. Nitoe ufanuzi kwamba wale watuhumiwa ambao wametajwa nao wanayo haki ya kuchangia. Kwa hiyo, wasije wakalamika kwamba tumehukumiwa bila kupewa nafasi ya kujitetea. Tunaendelea, Mheshimiwa Chitalilo atafuatiwa na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. Mheshimiwa Chitalilo endelea.

MHE. SAMWEL M. CHITALILO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa upande wangu kwanza nasikitika sana. Huwa siku zote tukija kuanza Bunge Asubuhi saa 3.00 huwa tunaanza kwa dua njema kabisa unayoiongoza wewe mwenyewe. Vile vile napenda tukumbushane kwamba yanayotokea, Mungu yupo kama tunavyoanza hapa Asubuhi.

Mimi kwa upande wa adhabu iliyotolewa kwa miezi sita hawa watu, yaani Mheshimiwa Ndassa pamoja na wengine kwamba wasifike hapa Bungeni, mimi binafsi sikatai adhabu hiyo, lakini napingana na muda. Ninaomba adhabu ipunguzwe. Kama Bwana Agustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa zamani wa Temeke, aliweza kutoa tuhuma za uongo na zikasababisha mtandao wa wasiwasi ndani ya Watanzania lakini bado alipewa adhabu ya siku 40, pamoja na hili la akina Ndassa kutetaa mtu ambaye ni Mbunge mwenzao na pamoja na uongo na kuisababishia Serikali hasara kiasi fulani, mimi sioni kwamba kuna sababu kubwa ya hasara hii. Lakini uongo ambao ulirindima na Taifa likapata wasiwasi nafikiri hiyo ndiyo ilitakiwa kuwa adhabu kubwa sana kuliko pesa. Kwa hiyo, mimi naliomba Bunge na ninaomba Wabunge wenzangu kwamba adhabu waliyopewa wenzetu ipunguzwe ibaki miezi mitatu au kipindi hili cha Bunge litakapokwisha, basi wenzetu wasiwe na adhabu tena. Ni ombi langu hilo. (*Makofit*)

Vile vile nitapenda kupata ufanuzi kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Madaraka ya Bunge, wakati anawasilisha hoja yake hapo amesema kwamba yeze alitaka suala hili alipeleke Mahakamani. Nataka ufanuzi kwamba yeze alitaka kulipeleka suala hili Mahakamani binafsi au Kamati imemwagiza au namna gani? Napenda nipate ufanuzi huo.

Vile vile la tatu, huu mtindo wetu wa Bunge hapa wa kuwa tunatoa mifano ya nchi nyingine lakini tukija kwenye maslahi ya Wabunge hapa kila siku wanapiga kelele kwamba walingane na Kenya na kadhalika. Lakini tukija kwenye matatizo mnalinganisha na nchi nyingine kwa nini? Ninaungana na hoja hii. Sina mengi. Lakini nitaungana na hoja hii asilimia mia baada ya kifungu walichopewa wenzetu kupunguzwa. (*Kicheko/Makofit*)

SPIKA: Mheshimiwa Mutungirehi ameshakwenda Mtera, hayupo. Mheshimiwa Ponsiano Nyami, atafatiwa na Mheshimiwa Esha Stima.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia. Kwanza ninaishukuru na kuipongeza Kamati kwa jinsi ambavyo ilichambua mambo haya kwa kina na kwa jinsi ninavyoifahamu Kamati hiyo, ni Kamati ambayo imetumia busara nyngi na bado itaendelea kutumia busara nyngi. Lakini Kamati hiyo hiyo ina watu wapole ambao wanajua kwamba kosa linaweza pia likawafika hata wao na vile vile Kamati hiyo inajua kutenda haki.

Lakini naomba tufahamu kwamba mara nyngi jambo linapoonekana kuwa kubwa watu wengine ambao wana miyo ya juu juu huwa waoga na huwa wanakwepa kusema ukweli na baadhi ya tabia ya watu wengine kutokuona umuhimu wa Vikao, pengine kukaa mpaka mwisho au kwa kipindi kirefu husababisha kuingia labda kwenye Kamati wakaweka sahihi na baadaye kuondoka. Ninahisi katika uchambuzi wa Kamati hii kama ilivyoelezea katika suala zima linalohusiana na kesi ile ya Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Dr. Kabourou pamoja na Mheshimiwa Dr. Kitine, inaonekana kwamba kuna watu walikwenda kuweka sahihi kutimiza wajibu wakaondoka na matokeo yake kwa vile umeshasaini na umeondoka, Kamati inaendelea kuwa ni halali. Kwa hiyo, mamuzi yatakayotolewa mwishoni yakiwa ni ya watu wachache yataendelea kuwa halali. Ninahisi ndicho kilichotokea.

Kwa mfano, kuwepo au kutokuwepo kwa kesi inayohusiana na Mama Kitine inawezekana ilikuwepo au haikuwepo lakini tatizo ni mahudhurio yaliyokuwepo. Kama watu walikuwa ni wachache na waliosaini ni wengi na wakawa wameondoka, wataendelea kukataa kwamba hoja hiyo haikuwepo wakiona kwamba kuna utata na pengine wanaoweza wakawajibishe na wale wachache waliokuwepo watakubali kwamba hoja hiyo ilikuwepo kwa sababu wao walishiriki. Kwa hiyo, mahudhurio nusunusu ndio madhara yake yanaweza kutufikisha hapa tulipo.

Jambo lingine ni zile kumbukumbu zinazofikiriwa kwamba zilighushiwa na Kamati inaonekana kukubali kwamba bila mashaka yoyote wanakubali kwamba kuna baadhi ya nyaraka zilighushiwa. Lakini wana ushahidi gani? Maana yake Tanzania tuna chombo kinachoitwa *Identification Bureau (IB)* cha Polisi ambacho ndicho chenye uwezo wa mwisho wa kutoa taarifa kwamba *document* hiyo ilighushiwa au *document* hiyo haikugushiwa. Je, Kamati inapofikia uamuzi kwamba *document* fulani inaonekana ilighushiwa, kuna mawasiliano yoyote na chombo chetu cha Polisi kinachoshughulikia masuala ya kugushi? Kama hayapo, basi Kamati haikupaswa kukubali moja kwa moja kwamba kuna maandishi yaliyogushiwa.

Wanasema, mtu muungwana ni mtu ambaye hukubali kosa na akaomba msamaha. Mheshimiwa Ndassa alipohojiwa kwenye Kamati, aliomba msamaha. Aliomba msamaha kama muungwana na kama binadamu kwamba kila binadamu hukosa na hata katika Mahakama unapoomba msamaha katika hatua ya mwisho, sina uhakika sana lakini nadhani kwenye *mitigation points* Mahakama inaweza ikafikiria kutoa adhabu kubwa, lakini baadaye Mahakama hiyo hiyo inaweza ikapunguza kosa kutohana na jinsi gani ulivyoomba msamaha na pengine kubembeleza.

Lakini wote kwa pamoja watatu, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Dr. Kitine na Mheshimiwa Dr. Kabourou, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Ibara ya 60(2) kosa lao ni la kwanza. Vile vile katika kifungu hicho cha 60 ambacho kinaelekeza adhabu zinazoweza kutolewa na Bunge ibara ya 60(2) inasema hivi, naomba kunukuu: "Kama hoja yoyote chini ya fasili hii itapitishwa na Mbunge kusimamishwa kazi, basi ikiwa ni kosa lake la kwanza ataendelea kuwa ameendelea kusimamishwa hadi kikao cha tano. Kama kosa la pili, hadi kikao cha 20; lakini kama kosa ni la tatu au zaidi, basi Mbunge huyo ataendelea kuwa amesimamishwa kazi hadi hapo Bunge litakapoamua kwamba kusimamishwa huko kwa Mbunge kukome." Mwisho wa kunukuu.

SPIKA: Nukuu na ya tatu, usiishie hapo. (*Kicheko*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako ninukuu kifungu kidogo cha tatu, kinasema hivi: "Bunge laweza kumchukulia hatua nynginez za kinidhamu Mbunge yeoyote aliyetenda kosa chini ya Kanuni hii kwa kumpitishia Azimio ambalo litataja hatua hizo zinazokusudiwa kuchukuliwa pamoja na sababu zake."

Mwisho wa kunukuu. Kosa hili ni kosa la kwanza. Nazingatia katika Kanuni hiyo kwamba kosa hili ni la kwanza kwa wote watatu. Nilikuwa naomba huruma ya Bunge hili sasa ione umu himu wa kuweza kufuata Kanuni ya 60(2) ili kusudi adhabu yao ipunguzwe.

Kwa kuzingatia kifungu kidogo hicho cha tatu, nilikuwa naomba adhabu yao iwe katika Bunge hili tu, maana kuwasimamisha kwa kipindi cha miezi sita, si tu kwamba unawaathiri wao wenyewe, lakini pia unawaathiri wananchi katika Majimbo yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge tunapaswa kuelewa kwamba kila binadamu sio mkamilifu na tunaambiwa hata malaika na wao sio wakamilifu. Ni makosa mangapi ambayo yametendwa na watu lakini yakafunikwafunikwa tu? Mimi nilikuwa naomba na kupendekeza kwa Waheshimiwa Wabunge hili kwamba adhabu waliyopewa ni kubwa sana, ninaomba muunge mkono hoja yangu kwamba ni katika Bunge hili tu ndilo waweze kusimamishwa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mutungirehi umerudi, basi nafasi yako ilishafika. Endelea kabla sijamwita Mheshimiwa Esha Stima.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kusema mawili matatu. Nadhani kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, mimi ni Mjumbe wa Kamati iliyohusika na tulikuwa na *hard time* kama ambavyo naiona hapa ilivyo kwa sababu wakati mwingine katika Mikutano mengine mnapotjadili mtu huwa wanamwambia atoke nje. Lakini hapa mnapotjadili mtu anakuona usoni inakuwia taabu kidogo. Kwa hiyo, napata shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna taarifa mbili. La kwanza alikuwa anasema Dr. Slaa kuhusu Mheshimiwa Ndesamburo. Sasa nadhani umeomba ufanuzi wa kisheria na sitaki kujielekeza huko tena. Wengi nadhani waliamua kwenye Kamati kama ilivyopendekezwa, ila kitu kimoja nilitaka tu nikiseme; katika yale ambayo tulipewa ya kwanza katika hii ya pili ya kuchunguza tuhuma zilizokuwa zinamkabili Mheshimiwa Ndassa, nadhani Kamati ilipoona kuna watu wengine kwenye mnyonyoro ule ilibidi na wao waingizwe na katika hili la Mheshimiwa Ndesamburo.

Ni bahati yake mbaya kwamba, hii nyingine tulitumia karibu wiki mbili, hii ya kwake nadhani tulitumia muda kidogo, lakini yeze ndiye nilikuwa nasema hapa kwamba *the intentional meaning* ya kitu fulani *and in the interpretation meaning* ya yule aliyeisikia. Kwa kuwa yalikuwa ni majibizano kwamba alimsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu akisema ukitaka mambo yako yakunyookee uingie CCM na yeze sijui akaongeza ya kwake ya *TRA*, basi tu lakini na mimi ningependa kushauri kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ashauriwe kwamba maneno ya viongozi unapoyasema wakati mwingine yanaweza kuleta mtafaruku kwenye jamii kwa sababu hata kule Rwanda wakati wanauana kuna mtu alisema maneno. Kwa sababu tukifika mahali mtu akifiwa usimzike kwa sababu sio wa Chama chako au kama mtu ana duka usiende huko kwa sababu sio wa Chama chako au mtu ana *Guest House* usilale mle kwa sababu sio wa Chama chako, nadhani nchi tutakuwa tunailekeza kubaya. Kwa hiyo, nadhani nimeeleweka nilichotaka kusema.

Mheshimiwa Spika, ya pili ni katika hii ya Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Dr. Kitine na Mheshimiwa Dr. Kabourou. Nadhani hoja ya msingi kama alivyoileza Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba Mama Saada Kitine alimwandikia Mwenyekiti wa *PAC* kwamba anaomba uamuzi uliokuwa umefikiwa wa kumpeleka Mahakamani usitishwe ili aweze kuendelea kulipa. Ndio ilikuwa ombi la Mama Kitine na tulitarajia watu wote waungane na kama wangelikuwa wanakubaliana na hilo iwe ndio agenda kwamba anaomba asije akapelekwa Mahakamani ataendelea kulipa hela za Serikali. Sasa kilichofikishwa kwenye Mkutano ule wa *PAC* sijui ulikuwa ni Mkutano hewa, sijui Mkutano wa nani? Maamuzi ilikuwa ni katika mambo mawili ambayo hayakuwa agenda kwamba asamehewe wakati hakuomba kusamehewe kwa kulipa lile deni na arejeshewe hela ambazo alikwishalipa vitu ambavyo hakuomba. Sasa katika mtataniko kama huu, unajiuliza aliyeleta lile wazo ambalo halikuwa kwenye barua ya mwombaji ni jini au ni mwanadamu? (*Kicheko*)

WAHESHIMIWA WABUNGE: Maruhani. (*Kicheko*)

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, hata akiwa maruhani au akiwa jini lazima tujilize ana sababu gani za kuingiza kile ambacho hakuombwa? Kulikuwa na sababu gani? Kulikuwa na nini huku nyuma? Ndio maana tunashangaa. Huyu mtu mzima ameandika barua anaomba mimi msinipeleke Mahakamani nitaendelea kulipa kama nilivyokwishesasema, wewe unasema asilipe halafu na zile alizokwishesazilipena zitafutwe haraka arejeshewe!

Mimi nadhani hatuwezi kukaa hapa tunafanya masuala ya mzaha, ndio maana tukafikia mahali tukasema tuwaite na bahati nzuri kama tulivyokueleza tulikuwa tunawaita wanakaa wanaangaliziana hebu wewe Dr. Kabourou mwulize Dr. Kitine.

Mimi Dr. Kitine nilikuja, hebu mwulize na huyu swali wanaulizana wanaangalizana ili mtu asije akamsingizia mwingine na tunamkumbusha wewe ulisema hivi juu ya huyu!

Mheshimiwa Spika, limegusiwa suala la kwamba binadamu, sijui binadamu anakosea. Unajua dhambi sio kutenda vibaya tu, dhambi ni kutokufanya vizuri wakati una uwezo wa kufanya vizuri. Huwezi kupita mahali nyumba inaungua na mtoto yuko ndani anataka kuungua, wewe unaiangalia unacheke unapita anaungua unaangalia halafu baadaye unakuja kwenye msiba kwamba nimeleta hela sijui za rambirambi, huwezi kufanya hivyo.

Kwa hiyo, tunachosema hapa ni kwamba wale wote ambao walipelekea kwenye hatua za kuhakikisha kwamba barua ile inakuja na wanaweka matatizo mengine ndio tunawashughulikia.

Mheshimiwa Spika, lilikuwepo suala la kugushi amelisema Dr. Slaa. Hapa zipo hatua mbili. Hatua ya kwanza ni ya kugushi muhtasari na ninaomba Mheshimiwa Dr. Slaa tuelewane kwa sababu yeye anajua kugushi. Ni kwamba Kanuni za kutengeneza mihtasari, mmejadili kwenye kikao, unaita kikao kingine mnasoma yatokanayo mnakubaliana, mnabadilisha maneno, mnabadilisha majina ndio haya tuliyosema Waheshimiwa Wajumbe? Ndiyo. Nitie sahihi? Ndiyo. Si ndiyo tunavyofanya? Sasa kama wewe unajipeleka mtu mmoja na hukuita Mkutano na unajisahihisha mwenyewe, unajirekebisha hivi hujagushi?

Mheshimiwa Spika, hili sidhani kama inabidi uende kuita vyombo vytaalam kuchunguza kwamba hivi inakuwa ni kugushi? Kwa sababu wewe ulipokonya na madaraka ambayo sio ya kwako. Hilo la kwanza. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa kipengele (b) katika kugushi ziko barua za Mama Saada Kitine. Kwa bahati nzuri Dr. Kitine ni rafiki yangu. Lakini alikuja na tukamwuliza na yeye akatueleza kwamba na yeye ana faili kama alilonalo mke wake na zile *correspondence* zote.

Wote waliokuwa wanaandika walikuwa wanampa mke wake kama yeye *addressee* wa kwanza na yeye wanampa nakala na akafika kutueleza kwamba na yeye alikuwa anamsaidia *ku-draft* baadhi ya barua na kumpa mawazo na zingekuwepo hapo mngejiridhisha kwa sababu watu wengine unaweza kukuta mimi nimeandika mawazo yangu kwenye karatasi ukasema haya ni ya Mutungirehi. Hii *tone* na hii aya ni ya Mutungirehi. Yeye mwenyewe tulipomwuliza akasema: "Mengine hayo mawazo kwa kweli ni ya kwangu hawezu kuiandika hivyo mke wangu".

Kwa hiyo, inapofika hapo yale tuliyoyasema sio kwamba tunataka kumwonea. Kwa hiyo, suala la kugushi na katika ushahidi anaousema Dr. Slaa nadhani wataalam wa sheria wako hapa, sio kwamba kila ushauri wa kitaalam baada ya mtaalam kuchunguza haya ataifanya Mahakama ikubaliane hivyo tu na mtaalam alivyofanya, vingine anaweza kuvikataa. Nadhani amaelewa hivyo.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea na suala lingine la mahudhurio nusunusu kwamba hawa walihudhuria baadaye wakaondoka kwa hiyo *iguarantee* kurejesha *agenda* ambayo haikuwepo, ni kitu ambacho sisi hatukukiona kama kinakubalika.

Mheshimiwa Spika, katika hili lingine ambalo amesema mzungumzaji mwingine la kutomwita Mama Kitine, kwa kweli kwa jinsi mzigo tuliokuwa nao na jinsi tulivyopata ule Ushahidi, kwa sababu sisi *concern* yetu haikuwa kama Mama Kitine na risiti zake, yake ilikuwa ni yeye na Serikali.

Tukubaliane, mimi ni Mbunge, nimewaambia watu mnichague nitakwenda nitawatetea, sasa leo hii mimi nimechukua hela za Serikali nimenunu tiketi ya *Air Tanzania* nikasafiri, nairejesha nasema mnirudishie hela zangu wananiambia umeigushi halafu mimi nanywea nasinyaa. Hivi unaniambia nitaweweza kuwatetea watu? Tiketi ile ni halali na mimi najua ni halali na nimewaambia watu nitawatetea, sasa nashindwa kujitetea.

Sasa katika hili la makarasi, zile risiti sisi hazikutuhusu kwa sababu mhusika mwenyewe Mama Kitine na Dr. Kitine mwenyewe ni watu ambao wanaoweza kuthibitisha kama kile walichokipata ni sahihi. Kwa hiyo, lilikuwa ni suala la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatukuona sababu ya kumwita mama wa watu na kuanza kumhangisha pale. Sisi tulichotaka ni kwamba aliomba kwamba mnisamehe msinipeleke Mahakamani niendelee kulipa, mtu mwingine akachomekea maneno hayo.

Kwa hiyo, si kwamba tulikataa kumwita kwa sababu tumevunja haki nyiningine na tukamtaja hapa.

Mheshimiwa Spika, *of course* hili la madawa, kulikuwepo na wataalam. Sasa kama yuko Daktari pale, Daktari pale, akawambia haya bwana hizi risiti zote ungenunu dawa zote hizi yatakuwa ni makopo kiasi fulani.

Sasa mtaalam huyo anajua makopo kiasi fulani yanatoka kwa Hospitali au yanawatosha watu 500. Sasa kama uliyameza mtu mmoja *definitely* nadhani itakuwa inatupeleka huko. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni vigumu kama tulivyosema kwamba ukikaa pale unataka kuwashukumu wenzako inakuwia vigumu, lakini sasa nani asiyemhukumu mwenzake? Kwa sababu *Judge* ni binadamu, ukiwa na kesi ya Ubunge atakuhukumu na hatakuogopa kwa sababu na yeye baadaye anaweza akagombea.

Mheshimiwa Spika, *administrator* yelete, atakuhukumu tu. Lakini kwa sababu tumewekwa kwenye Kamati hii hatuwahukumu kwa kuwakandamiza na sisi tunacho sema ni kwamba mara nydingi hata hizi adhabu za kifo ambazo nchi nyiningine wanazipigia kelele, yule aliyeua wanasema au auawe, mara nydingi *intention* yake siyo kumfundisha yeye. Kwa hiyo, tunaona watu wanajibamiza anasema nitakuwa na mimi naua. Ni kuwafundisha wale waliobaki kwamba ukifanya mambo ya ovyo ovyo watakuua. Sasa wale waliobaki wanakuwa na woga.

Sasa katika hii, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, anatuhumiwa alisema uongo hapa wa kutafsiri vibaya maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, "wote muingie CCM mambo yatawanyookea." Miezi miwili, watu wale wale kwa sababu tunachotaka kufanya ni kwamba jamii ituelewe tunachofanya ni nini. Wewe umeghushi, ume-*conspire*, umepoteza fedha za Serikali, unavunja utaratibu, makosa matano. Halafu mnataka kuwalinganisha wote hawa. Mimi sikubaliani na hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa natoa nafasi kwa watuhumiwa walioomba kuchangia. Naanza na Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuata Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie haya yaliyo mbele yetu. Lakini awali ya yote naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili pamoja na Wajumbe wake wote. Najua ni watu makini, wamekaa na wakaamua kama walivyoamua na sisi au mimi kama mtuhumiwa, nilipoitwa mara ya kwanza na ile mara ya pili, nilikiri

mapungufu yaliyojitokeza, kama binadamu, nilisema kabisa kwamba si nia yangu kufanya hivyo, lakini kama binadamu na kwa sababu ni mara ya kwanza tunajifunza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuititia Bunge lako Tukufu, wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Wabunge wenzangu, niwaombe samahani sana, kwa usumbufu wowote unaojitokeza hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na kama nia ya Waheshimiwa Wabunge wote, wale waliosema na wale ambao hawajasema neno, lakini walikuwa na nia ya kusema, ni kweli mimi yapo mapungufu ambayo niliyatenda na niseme tu wazi kwamba suala la kughushi mimi nasema siyo sahihi, labda neno lilitumika vinginevyo. Lakini mimi nilipokea taarifa ile na tukaipitia kwa utaratibu mzuri kabisa. Lakini nisingependa Bunge lako Tukufu ku lirudia tena huko tulikotoka, nisingependa. (*Makofi*)

Kwa sababu Kamati ya Mheshimiwa Eliachim Simpara, imenihoji mara mbili. Nikaitwa tena mara ya tatu, nikasema kabisa jamani, mimi ni binadamu, hayo niliyofanya jamani, Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba mnisamehe kwa nia nzuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, adhabu niliyopewa mimi siwezi kuikataa, lakini ni Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Spika, ndilo lenye uwezo na madaraka ya kusema basi kwa sababu ni mara ya kwanza, nimekaa huu ni mwaka wa nane na sina ugomvi na Mheshimiwa Mbunge ye yole humu ndani. (*Makofi*)

Sijalikosea Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Spika. Hata wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, nimekuwa mtiifu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Naomba Bunge lako Tukufu, kwa imani naomba adhabu hii ikiwezekana ipunguzwe, ikiwezekana basi iondolewe kabisa, iwe ni fundisho. Vinginevyo nipewe onyo kali. (*Makofi*)

Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

MHE. DR. AMANI W. A. KABOIROU: Ahsante Mheshimiwa Spika, mimi niungane na Mheshimiwa Richard Ndassa, kwa yale aliyojasema. Lakini niseme tu kwamba mimi nakubali adhabu kama ndiyo njia ya pekee ya kuendelea kuyafumbia macho makosa ya Serikali. Kwa hiyo, kama kweli tunataka kutenda haki Bungeni basi naomba Waheshimiwa Wabunge, tutafakari kwa kina kabla hatujapitisha mapendekezo ya Kamati hii.

Ahsante sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

SPIKA: Basi! Bado tunao muda Mheshimiwa Esha Stima, nadhani atakuwa ndiyo msemaji wa mwisho. Halafu tutahirisha Bunge majibu yatatolewa mchana.

MHE. CHIFU ABDALLAH S. FUNDIKIRA: Taarifa Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Sasa nitakuja kwako. Taarifa kwa nani? Kwa sababu taarifa lazima itolewe kwa maelekezo. Endelea Mheshimiwa *Chief Abdallah Fundikira*.

MHE. CHIFU ABDALLAH S. FUNDIKIRA: Katika shughuli kama hizi ama inapolazimu kutoa adhabu na mambo kama hayo. Naomba unifafanulie anayetoea adhabu ni Bunge ama ile Kamati ambayo inapendekeza?

SPIKA: Ndiyo, ufanuzi ni kwamba anayetoea adhabu ni Bunge. Kamati inafanya kazi za awali, inaleta mapendekezo. Sasa Bunge linakubaliana au linakataa mapendekezo hayo. Mwenye kutoa adhabu ni Bunge lenyewe.

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi ya kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchangano wangu kuhusu hoja hii iliyokuwa mbele yetu.

Mimi kwanza nampongeza Mwenyekiti na Kamati yake kwa kazi makini waliyoifanya katika kuchunguza ukweli wa makosa waliyofanya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine. Kwa kweli mimi naunga mkono adhabu iliyotolewa na Kamati. Lakini nilikuwa na ombi maalum katika suala hili na hasa tukikumbuka kwamba makosa hufanywa na binadamu wote.

Hata huko nyuma, viongozi wetu wa nchi hii waliwahi kuwasamehe watu ambaao walifanya makosa makubwa kabisa ya kukusudia kuwaa na kupindua Serikali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa walikusudia kumwaga damu ya viongozi na pia wananchi ambaao wangepata msukosuko kipindi kile, Mheshimiwa Marehemu Mzee wetu Mwalimu Julius Nyerere, aliwasamehe wale ambaao walitaka kupindua Serikali yake na kumuua, siyo kupindua tu na kuuuua. Alitoa msamaha. Kwa misingi hiyo basi, nilikuwa naiomba Kamati, Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tukubali wenzetu hawa wapunguziwe adhabu. (*Makofi*)

Kama kutakuwa na uwezekano Mheshimiwa Spika, basi Bunge hili linawatosha kabisa kutokuwepo kwao ni adhabu tosha na watakumbuka maishani mwao kwamba sitorudia, hawatarudia tena kosa la aina hiyo katika maisha yao wakiwa kama viongozi. (*Makofi*)

Hilo ni ombi kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge. Lakini pia nilikuwa naomba Mheshimiwa Spika, niombe pia msamaha kwa Katibu Ndugu Elisa Mbise. Kwa sababu na yeze pia ni kosa lake la kwanza. Yeze ana adhabu ya kuandikiwa barua ya onyo kali. Kwa kweli kiutumishi onyo kali ni karibu na kifo chake na kwa vile kiutumishi nasema, siyo kifo chake kwenda kuzikwa, kiutumishi, baada ya hapo akifanya kosa lingine hata kama ni dogo tu anaweza akafukuzwa kazi. Nasema hivyo, kwa misingi gani Mheshimiwa Spika? Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge au watumishi wa Bunge hawawezi kubishana na Mheshimiwa Mbunge hata siku mmoja. (*Makofi*)

Wanapoagizwa kwamba tenda hiki, wao sawa Mheshimiwa. Tunawaona hapa. Kwa misingi hiyo, yeze asingeweza kusema kwamba mimi sitaandika hili na wala sitalifanya hili nakwenda kwa mkubwa wake. Kwanza yeze hakujuua kwamba kuna njama ya aina yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili lazima tulifahamu na Waheshimiwa Wabunge kwamba kijana huyu hakufanya kosa alilolifahamu. Tunaomba asamehewe na asiandikiwe barua ya onyo kali, kwa sababu ni hatari kiutumishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitaki nirudie waliyosema wenzangu, nayaunga mkono kwa misingi ya kupunguza adhabu na pia kusamehewe kijana huyu. Nashukuru kwa nafasi uliyanipa. (*Makofi*)

MHE. DR. HASSY H.B. KITINE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo tu na kwa kifupi sana. Nadhani ni *natural* kwamba Waheshimiwa Wabunge walitegemea na mimi niseme hata kwa dakika moja au mbili. Nilikuwa nataka kunyamaza kwa kweli Mheshimiwa Spika. Lakini nikaona baada ya michango ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia na Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou na Mheshimiwa Richard Ndassa, ambaao ndiyo watuhumiwa wenzangu, baada ya kuchangia na mimi nimeona nichangie kwa kifupi sana.

Kwanza, ninaomba na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati yake iliyotuita na kutuhoji kwa uwazi na uadilifu kama alivyosema. Napenda kuwapongeza wote kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Pili, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Richard Ndassa na yule kijana Elisa Mbise, ambaye ni mwanafunzi wangu mimi, nilimfundisha Chuo Kikuu, ninaomba ieleweke kwamba hawa viongozi wawili na Mtendaji mmoja kwa kweli wanapata adhabu, Bunge hili litakuwa linawapa adhabu kwa sababu yangu mimi. (*Makofi*)

Nimesema *privately* kwamba ni bahati mbaya sana kwamba hili jambo limeweza kwa kweli kuwasumbua hawa Waheshimiwa Wabunge pamoja na yule kijana ambaye naye anapata adhabu hii ya kuonywa.

Sasa nataka kusema hivi, yote yaliyotokea huko nyuma kwa kweli sitaki, hayana maana yoyote kwa maana ya shughuli za nchi yetu na maana ya uwajibikaji. Mimi kama kiongozi na wenzangu wengine kama viongozi, ninachoomba ieleteke Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu, si rahisi kwangu mimi kuanza kusema yule mama alitibiwa na hivi ameonewa. Marekani haiwezekani mtu kama ni mgeni akalipia na Bima ya kule, haya mambo yako huko na *in facts*, lakini sitaki kurudi huko nyuma kwa sababu hakusaidii kitu chochote, haisaidii Bunge letu wala haisaidii nchi yetu kwa kweli.

Sasa hali ilivyo ni kwamba iwe Mama Kitine na kwa kweli Serikali ilimsaidia sana. Mama Kitine yeze anajielewa kama aliugua ama hakuugua. Kuna *claim* kwamba *in fact* hizo pesa alikula kwa sababu wala hakuugua. Sasa hii anajua yeze mwenyewe zaidi. Lakini mimi ninachoomba hapa, *all said and done* mimi ninaomba kwa niaba ya Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Richard Ndassa na Bwana Elisa Mbise, kwa kweli na nilisema katika Kamati kwa kweli nasikitika, lazima niseme nasikitika kweli kwamba hawa watu wanapata adhabu kwa sababu yangu mimi na Mama Kitine.

Mheshimiwa Spika na mimi kwa kumalizia naomba niseme kwamba, *impression*, iliyokuwa *created* pamoja na taarifa nzuri kabisa ya Kamati, *impression* iliyokuwa *created* hapa ni kama kulikuwa na *some conspiracy*, kulikuwa na mbinu ambazo mimi nilifanya, kwa kuwa mimi ndiyo Mtuhumiwa Mkuu.

Ninaomba Mheshimiwa Spika, ninasema hivi, pengine si sahihi sana ukiwa ndani ya Bunge, tunapozungumza ndani ya Bunge kuzungumza habari ya Mungu. Mimi nasema Mungu anajua na yeze ana uwezo wa kuhakikisha na kurekebisha mambo hapa hapa duniani.

Sasa kama kulikuwa na *conspiracy* au ujanja ujanja wowote na ujanja huu *source* lazima ilikuwa ni mimi. Kwa sababu mimi ndiyo niliywafanya hawa Mabwana, Mheshimiwa Spika, samahani nikawaghiribu mpaka wakataka kuanza kufanya mambo ambayo nataka mimi. Lakini nataka kusema yote ninaacha na inajulikana huko mbele ya safari, mbele ya Mungu.

Mheshimiwa Spika, lakini *facts* kama zilivyotolewa hapa, basi Mheshimiwa Spika, tunazikubali hizo na mimi nakubaliana na adhabu iliyotolewa, ndiyo adhabu sahihi ambayo Kamati imeona ndiyo adhabu sahihi.

Sasa kama Bunge litakuwa linafikiria kupunguza au kuongeza inawezekana kabisa, Bunge likaona kama hii adhabu haitoshi. Mimi niko tayari kuichukua hiyo adhabu kwa mikono miwili, nitakwenda Makete, nitawaambia wananchi jamani tuko wote miezi sita safari hii, mtaona vikaoni siendi huko kwa sababu hali ilivyo ndivyo ilivyo kwa sababu siwezi kuficha.

Naomba Mheshimiwa Spika, nirudie kwamba *there was* *absolutely no conspiracy at all*. Lakini ningeomba ieleteke hivyo Mheshimiwa Spika. Ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea. Ahsante sana. (*Makofsi*)

WABUNGE FULANI: Msamaha.

MHE. DR. HASSY H. B. KITINE: Msamaha nilidhani ndiyo nimeomba hivyo. Sasa sijui maana yake, sikutumia neno msamaha. Ninaomba msamaha kwa Bunge lote. Nilidhani niliomba, kumbe sikuomba.

Mheshimiwa Spika, ninaomba msamaha *formally* kwa kuwavuruga Waheshimiwa Wabunge, wamepoteza saa mbili kwa kuzungumza habari ya mke wangu. Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. (*Makofsi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mjadala huu sasa umefikia mwisho. Tutakaporejea mchana kabla mtoa hoja hajapewa nafasi ya kuhitimisha, tutapata ufanuzi niliouomba wa Kisheria kutoka kwa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lakini kabla ya mto hoja kujibu, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kwa mujibu wa Kanuni zetu ameleta hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja hii.

Napenda niwaarifu ili twende mapumzikoni tukijua kwamba hii nayo itawasilishwa Bungeni. Ni hoja ya kubadilisha pendekezo la Kamati.

Pendekezo la Kamati ni kwamba hao Wabunge watatu, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou na Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, pendekezo linasema, wapewe adhabu ya kusimamishwa kazi ya Ubunge kwa muda wa miezi sita kuanzia tarehe ya Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Ponsiano Nyami, anataka kuleta pendekezo la mabadiliko linalosema, wapewe adhabu ya kusimamishwa kazi ya Ubunge kwa muda wote wa Vikao vya Bunge hili linaloendelea kuanzia tarehe ya Azimio la Bunge hili, ni hoja ya mabadiliko anayotaka kuileta, tutaijadili mchana. Kwa hivi sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. (*Makofi*)

(*Saa 6.50 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kikao kilichositishwa Saa 7.00 mchana kinaendelea. Kama nilivyoeleza wakati wa kusitisha shughuli za Bunge kwamba tumepokea taarifa ya mabadiliko ya hoja iliyowasilishwa, ni lazima itolewe kabla mto hoja hajahitimisha.

Kwa hiyo, sasa namwita mto hoja ya mabadiliko ili aweze kuwasilisha hoja yake.

**HOJA YA MABADILIKO KUHUSU ADHABU ILIYOPENDEKEZWA KUTOLEWA KWA
WABUNGE WALIOSIMAMISHWA**

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi tena ili kusudi niweze kutoa hoja yangu ya mabadiliko katika hoja iliyotolewa leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya utaratibu wa leo si ule amba tulikuwa tumeuzoea ambao mara nyingi huwa tunapewa nyaraka tu mara tu *Order Paper* inapokuwa imekwishatoka, kwani kwa kufanya hivyo inakuwa ni rahisi sana kwa Waheshimiwa Wabunge, kuititia hoja inayohusika na kwa maana hiyo kuweza kuishauri Kamati inayohusika kikamilifu. Kwa hiyo, ilikuwa ni vizuri tangu wakati ule *Order Paper* ilipokuwa imetoka asubuhi, ilikuwa inatakiwa tuwe tumeshapewa hiyo ili Waheshimiwa Wabunge waipitie kwa muda wa kutosha.

SPIKA: Siyo hayo unazungumzia mabadiliko katika Miswada ya Sheria.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Baada ya kusema hayo...

SPIKA: Aah usiseme baada ya kusema hayo, sema umesikia maelezo.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Nimesikia maelezo. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa kutumia Kanuni Na. 47 ya Kanuni za Bunge katika taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kuhusu uchunguzi juu ya maamuzi ya kufuta hoja ya Mama Saada Kitine na kusamehe deni la Serikali la dola 63,450.

Kuhusu Kifungu cha 4(1), adhabu zilizopendekezo ni kwamba ninaomba kufanya mapendeleko ya kufuta maneno yafuatayo: "Wapewe adhabu ya kusimamishwa kazi ya Ubunge kwa muda wa miezi sita kuanzia tarehe ya Azimio la Bunge hili." Naomba maneno hayo yafutwe na badala yake yawekwe maneno yafuatayo: "Wapewe adhabu ya kusimamishwa kazi ya Ubunge muda wote wa Vikao vya Bunge hili vinavyoendelea kuanzia tarehe ya Azimio la Bunge hadi tarehe 7 Agosti, 2003.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niwe mchangiaji wa kwanza katika hii hoja ya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami. Sina jipyâ nitakalolizungumza bali ni kurudia yale ambayo waliyazungumza wenzetu asubuhi, kwamba kipindi cha miezi sita ni kipindi kirefu kama wenzetu wasasimamishwa kwa muda huo. Hawataathirika wao tu bali wale watu wanaowawakilisha watakuwa wameathirika sana na kwa sababu binadamu ana mapungufu mengi, yejote kati yetu anaweza akafanya makosa wakati wowote na kwa sababu kosa lao ni la mara ya kwanza, basi mimi naunga mkono kwamba adhabu yao ibadilishwe toka miezi sita mpaka katika hiki kipindi cha kuanzia tarehe ya hii adhabu au pendekezo liliyotolewa mpaka mwisho wa Bunge hili ambayo ni tarehe 7 Agosti, 2003. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii.

SPIKA: Shukrani. Kuna anayetaka kuchangia kupinga hoja hiyo?

WABUNGE FULANI: Hamna.

SPIKA: Hamna! Basi tusipoteze muda wa Bunge. Hoja inalenga kubadilisha adhabu iliyopendekezwa na Kamati kwa Wabunge watatu walijotajwa kutoka miezi sita kuwa ni kuanzia mkutano huu mpaka mwisho wa mkutano huu wa Bajeti.

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Hoja ya Mabadiliko Kuhusu Adhabu Iliyotolewa kwa Wabunge Waliosimamishwa Ilikubaliwa na Bunge*)

SPIKA: Kwa hiyo, sasa mto hoja atahitimisha hoja yake kama ilivyobadilishwa na Bunge.

Lakini kabla sijamwita napenda nitoe maelezo kwamba, katika hoja iliyowasilishwa ametajwa mtu ambaye si Mbunge ni mtumishi. Utamaduni wa Mabunge mengi ya *Commonwealth* huwa unakataza watu wasioweza kujitetea Bungeni mambo yao yasizungumzwe.

Sasa mambo ya watumishi wa Wabunge yanasisamawi na Tume ya Huduma za Bunge si Bunge kama Bunge linapokaa katika utukufu wake.

Kwa hiyo, mimi ningependekeza wakati Mheshimiwa mto hoja unapowasilisha, badala ya kupendekeza kwamba Bunge hili ndiyo litoe adhabu kwa mtumishi huyo, ni vizuri upendekeze kwamba suala la adhabu ya mtumishi huyo lipelekwe kwenye mamlaka inayosimamia nidhamu za watumishi. (*Makofî*)

Kulikuwa na suala la ufanuzi wa Kisheria, ni kweli. Sasa namwomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atufanulie kama kuna jambo lililopo mbele ya Mahakama sasa hivi ambalo linatuzuia sisi tusilijadili.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunitambua. (*Kicheko*)

Pili, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii kwa kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri iliyofanya kwa taarifa zote mbili.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alipokuwa anachangia hoja inayomhusu Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, alitoa wasiwasi wake, hisia kwamba, si busara kwa chombo kikubwa kama hiki kukiuka Kanuni zake na akatukumbusha kwamba Kanuni ya 50(3) inapiga marufuku kabisa kwa Mbunge yejote kuzungumzia jambo lolote ambalo linangojea uamuzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swal ihi, napenda tu tusaidiane kwamba Waheshimiwa Wabunge waelewe ni nini kilichotokea tangu tulipotoka kwenye Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Aprili, 2003 Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, kupitia Wakili wake, aliwasilisha maombi Mahakama Kuu ya kupewa ruhusa yaani *Application for Leave* ya kuweza kuwasilisha maombi ya amri tatu.

Mheshimiwa Spika, amri ya kwanza, ni hii Wanasheria wanaita *certiorari* lakini maana yake ni kwamba, uamuzi uliofanywa na chombo fulani uweze kuhojiwa na ikiwezekana ufutwe. Sasa hapa ilikuwa ni mwenendo wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ndiyo yalikuwa maombi yao ya kwanza kwamba mwenendo huo uletwe mbele ya Mahakama Kuu na uweze kufutwa.

Ombi la pili, lilitaka kuzuia Kamati hiyo isiweze kuwasilisha taarifa yake iliyofanywa kuhusiana na uchunguzi wa madai aliyotoa humu Bungeni Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, kwamba Kamati isiweze kuwasilisha taarifa yake. Hiyo ni kwa ombi la pili yaani *order ya prohibition* kukatazwa kabisa, amri ya katazo.

Ombi la tatu, lilihusu amri ya *mandamus* ambayo iliwataka walalamikiwa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, waheshimu sheria, waliona kwamba sheria hazikufuatwa ingawa hakusema ni zipyi. Lakini hayo ndiyo yalikuwa maombi ya msingi ambayo waliyaombea ruhusa, ndiyo taratibu za Kimahakama ili uweze kuwasilisha hayo. Hiyo ilikuwa tarehe 30 Aprili, 2003 lakini tarehe 6 Mei, 2003 wakawasilisha pia Mahakamani wakiiomba Mahakama Kuu itoe pingamizi la muda ili kuwazuia walalamikiwa, Spika na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pingamizi la muda (*Temporary Injunction*), wakasema *temporary prohibition injunction*. Hayo ndiyo maombi yao yalivyokaa.

Mheshimiwa Spika, lakini wazuiwe hao walalamikiwa wasipokee taarifa ya Kamati, wasipokee taarifa hiyo. Pili, wasichapise taarifa hiyo. Tatu, wasiruhusu taarifa hiyo kujadiliwa na Bunge au na chombo chochote cha Bunge kwa maana ya Kamati hadi hapo maombi yao yaliyo mbele ya Mahakama yatakopokuwa yamesikilizwa. Sasa hilo ni ombi lililowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa taratibu za Kimahakama ombi hilo la pingamizi ndiyo unaanza nalo kwa sababu wana sababu kwa nini wanataka wawahishe kabla ya ombi lao la ruhusa ya *application* ya *leave*. Siku ile ya tarehe 6 Mei, 2003 wakati anawasilisha ombi la pingamizi hilo, walisema kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwa hana haki, hana ubavu wowote ule wa kuweza kumtetea Mheshimiwa Spika, wakasema Spika akatafute Wakili wa kumtetea. Lakini na sisi hapo hapo tulitoa hoja zetu kusema kwamba, Mwanasheria Mkuu ana haki kabisa ya kumtetea Spika na utaratibu huo sio wa hapa tu lakini ni ndani ya nchi za Jumuiya ya Madola. Pale pale tukasema kwamba kwa yote ambayo yameletwa mbele ya chombo hicho cha Mahakama, Mahakama kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 100 haikuwa na haki, uwezo na mamlaka ya kuweza kuyasikiliza maombi hayo na tuliomba Mahakama iyafukuze maombi yaliyowasilishwa mbele yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Juni, 2003 Mahakama Kuu ilitoa uamuzi wake na kukubaliana na hoja za Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba Mwanasheria Mkuu ana haki ya kumtetea Spika. Pili, kwamba Mahakama Kuu haina mamlaka ya kusikiliza mambo yaliyowasilishwa Mahakamani na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku hiyo hiyo Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, kupitia Wakili wake, aliwasilisha maombi ya mdomo ya ruhusa yaani *Application for Leave to Appeal* mbele ya Mahakama Kuu na Mahakama ikamwambia Wakili tufuate utaratibu unaokubalika kwa kuleta *Application* ya *Chamber Summons* kwa njia ya *Chamber Summons*, ndiyo utaratibu unaokubalika. Siku hiyo basi tarehe 6 Juni, 2003 Wakili wa Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo ndiye aliyewasilisha taarifa ya kusudio la kukata rufaa (*Notice of Intention to Appeal*) na hapo hapo akaomba apewe nakala ya mwenendo wa shauri hili pamoja na nakala ya uamuza wa Mahakama Kuu iliyoutoa siku hiyo.

Sasa huo ni utaratibu na wakati hoja hii inaendelea ndiyo maana uliniona nimetoka kidogo nikai-alert system kule Dar es Salaam ili tuwe na uhakika wa kile ambacho kilitolewa hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kufika saa 9.30 wakati Masjala ya Mahakama ya Rufaa ilipokuwa inafungwa leo Mjini Dar es Salaam, hapakuwa na rufaa rasmi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, kupitia Wakili wake au Mawakili wake. Nilitegemea wao au Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alipokuwa anatoa rai yake hiyo kwamba angelithibitisha, angekwenda mbali kidogo kwa sababu tuna utaratibu kwamba unapowasilisha rufaa kwa Kanuni ni lazima Hati ya Rufaa iwepo, uiwasilishe Mahakamani *Memorandum of Appeal*. (*Makofi*)

wowote ule wa kuweza kumtetea Mheshimiwa Spika, wakasema Spika akatafute Wakili wa kumtetea. Lakini na sisi hapo hapo tulitoa hoja zetu kusema kwamba, Mwanasheria Mkuu ana haki kabisa ya kumtetea Spika na utaratibu huo sio wa hapa tu lakini ni ndani ya nchi za Jumuiya ya Madola. Pale pale tukasema kwamba kwa yote ambayo yameletwa mbele ya chombo hicho cha Mahakama, Mahakama kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 100 haikuwa na haki, uwezo na mamlaka ya kuweza kuyasikiliza maombi hayo na tuliomba Mahakama iyafukuze maombi yaliyowasilishwa mbele yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Juni, 2003 Mahakama Kuu ilitoa uamuza wake na kukubaliana na hoja za Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba Mwanasheria Mkuu ana haki ya kumtetea Spika. Pili, kwamba Mahakama Kuu haina mamlaka ya kusikiliza mambo yaliyowasilishwa Mahakamani na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku hiyo hiyo Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, kupitia Wakili wake, aliwasilisha maombi ya mdomo ya ruhusa yaani *Application for Leave to Appeal* mbele ya Mahakama Kuu na Mahakama ikamwambia Wakili tufuate utaratibu unaokubalika kwa kuleta *Application* ya *Chamber Summons* kwa njia ya *Chamber Summons*, ndiyo utaratibu unaokubalika. Siku hiyo basi tarehe 6 Juni, 2003 Wakili wa Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo ndiye aliyewasilisha taarifa ya kusudio la kukata rufaa (*Notice of Intention to Appeal*) na hapo hapo akaomba apewe nakala ya mwenendo wa shauri hili pamoja na nakala ya uamuza wa Mahakama Kuu iliyoutoa siku hiyo.

Sasa huo ni utaratibu na wakati hoja hii inaendelea ndiyo maana uliniona nimetoka kidogo nikai-alert system kule Dar es Salaam ili tuwe na uhakika wa kile ambacho kilitolewa hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kufika saa 9.30 wakati Masjala ya Mahakama ya Rufaa ilipokuwa inafungwa leo Mjini Dar es Salaam, hapakuwa na rufaa rasmi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, kupitia Wakili wake au Mawakili wake. Nilitegemea wao au Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alipokuwa anatoa rai yake hiyo kwamba angelithibitisha, angekwenda mbali kidogo kwa sababu tuna utaratibu kwamba unapowasilisha rufaa kwa Kanuni ni lazima Hati ya Rufaa iwepo, uiwasilishe Mahakamani *Memorandum of Appeal*. (*Makofi*)

Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine na Mheshimiwa Andrew Chenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuandika ni Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Mgana

Msindai, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Paul Ntwina.

Kwa hiyo, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa na *interest* ya kuchangia hoja hii ya aina yake.

Mheshimiwa Spika, nimefupisha sana michango yote ambayo imetolewa, kwanza, karibu kila mchangiaji aliunga mkono hoja, kasoro mtu mmoja tu ambaye alichangia kwa maandishi na alikuwa mkali kweli kwa maandishi, akasema siungi mkono hoja, huu ni ubinadamu gani, ametufokea sana kwenye Kamati.

Kwa hiyo, Mheshimiwa huyo naye ametumia haki yake. Mheshimiwa Sophia Simba, amesema tumewadhalilisha wenzetu kwa nini tunayasema mambo hapa hadharani labda tungCAA kwenye kificho na nini. Sasa Mheshimiwa Rais wetu anaongea juu ya uwazi na ukweli. Huyo peke yake ametushambulia kwa kweli, barua yake ninayo hapa toka mwanzo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo limejitokeza ni kwamba baadhi wamesema adhabu ipunguzwe na kwa kweli hao ni wengi.

Mheshimiwa Spika, tatu, kwamba ni kosa la kwanza kwa hiyo tutumie Kanuni ile ya siku tano na kadhalika na sisi tukasema sisi tulikuwa tumeng'ang'ania kwenye ile fasili ya tatu (3) na ya 61 kama ulivyotusaidia. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, nne, kwamba suala la kugushi lingeperekwa *IB* na pale ndipo namshukuru sana Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, amesema kama mtu ameghushi muhtasari, tunaeleza muhtasari umeandikwa nje ya kikao labda kama ntu hajui maana ya kughushi. Tumesema majina yameandikwa watu ambao hawakuwepo, sasa unataka asaini tu ndiyo maana ya kughushi? Si vizuri na ujanja mwingu huondoa maarifa.

Kwa hiyo, sisi hiyo ya kusaini ni kitu kidogo sana kwa sababu yule anaweza akaangalia akasema vinafanana, hii sahihi na hii ni sawa sawa, lakini sisi *actually Kisheria is not even binding* yale atakayoyapata yule *IB* siyo *binding* Kisheria, siyo lazima tuyafanyie kazi, sisi tunaona sahihi ni kubwa na imekaa tofauti na hii na kila mmoja anaona. Sasa kama watakwendu kule wapeane chochote halafu waseme ni sahihi tutafanyaje na sisi tunaona hizi ziko tofauti. Sisi tunachoona ni kwamba Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, hakuwepo na akina Mheshimiwa Estherina Kilasi hawakuwepo na Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira amesimama kwenye kikao akasema hawa walikuwa kwenye Bodi ya *National Freight Bureau* na hiki ni kitu ambacho kiko wazi, *minutes* hazikuandikwa, hivyo watu hawa wameandika porini porini tu na wamesaini. Tukumbushane Mheshimiwa, Katiba inasema nini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, hiyo ni Ibara ya 63, fasili ya (b). Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii. Watu wanaoweza kufanya mambo haya ninayoyasema ndiyo kazi waliyotumwa, si jambo dogo? Ukipenda mtoto mchape kama anakosea, wote waliowalea watoto kwa lelemama, watoto wale walikuwa siku chache baada ya wazazi wao kufa, wale ambao wamewalea kwa viboko hata kama baba akifa, lakini wanajitegemea.

Mimi, Mheshimiwa Richard Ndassa, *is my best friend* na ananipa shikamoo, anasema shikamoo mwalimu, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, ni rafiki yangu sana tena na mwenyewe anajua, yuko pale anafurahi, Mheshimiwa Philimon Ndesamburo, tunataniana huwa namwambia nitakuja Moshi siku moja ili nikutembelee, ni uongo Mheshimiwa Philimon Ndesamburo? Yuko hapa na Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, ni rafiki yangu tena najua anatoka Kijiji gani, tunaelewana sisi wenyewe, bahati ni kwamba ni kipaji ambacho Mungu anakupa kama wenzako wanakupenda.

Katika Bunge hili ninafikiri wote ni marafiki zangu lakini inapofika katika kutekeleza matakwa ya nchi, hayo mimi naweka kando, hamuwezi watu mlionopa hapa kwamba nitaitetea na kuilinda Katiba hii

mkae kantini mnaandika *minutes* ambazo hazipo, hamuwezi, mtakuwa ni watu wa ajabu sana, hivi itakuwa ni nchi ya namna gani?

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho hakikuwepo kinakuwa *cooked kabisa*, kitu kimeshamalizika na katika hili mtu alipoteza nafasi ya Uwaziri, si jambo dogo ila tatizo ni tafsiri ya uzito wa kitu katika maisha ya binadamu. Wengine wanaona jambo hili ni zito na wengine wanaona ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, mimi huwa nawatania sana watu wa Morogoro kwa sababu nimesoma kule na nimekulia kule. Yuko kiongozi mmoja aliniambia yule mtu wenu anawakemea sana Wakuu wa Idara halafu maneno yake ni ya utani utani, uswahili swahili na nini kwa hiyo, naona hafai tumtoe, nikasema hapana, nikamwuliza wewe unawafahamu Waluguru? Nikamwambia unamfahamu Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, akasema eeh, nikamwambia huwa unaskia anavyojibu maswali Bungeni? Ni kwamba yeze anacheka na kufurahi lakini ndiyo anajibu hivyo.

Nikamwuliza tena, unamfahamu Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, akasema eeh, anapojobu maswali unamwonaje na je, Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira? Wao wanaongea huku wanacheka, wanaendelea. Lakini Eliachim Simpara, sasa akisimama kwanza akunje uso, aonekane kama Muisraeli hivi, inategemea *seriousness* unaiweka wapi wewe. Katiba inalipa Bunge cheo kikubwa namna hii halafu mtu akakae kantini aanze kuandika na kusaini halafu unasema aah jamani!

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo iliyoua makampuni na mashirika yetu ya umma, watu wanasema aah ni mwenzetu au ni mtoto wa fulani jamani, kampuni inaanguka, ni mwenzetu au ni mtoto wa fulani, mwisho kampuni na mashirika yote ya umma yakaisha na sasa Serikali inabinafsisha tunaanza kuja juu aah lakini haya mambo leo yamezidi lakini tunafanyaje, tuwarudishe wale wale? Mimi tulikutana na Mheshimiwa Richard Ndassa, pale nikasema kwa kweli Mheshimiwa Richard Ndassa, wewe umepata adhabu inayostahili lakini wewe pengine ndiye umesababisha wenzako wapunguziwe adhabu kwa sababu wewe ulionekana mwadilifu na ulikuwa mnyenyekevu na uliomba radhi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hii Katiba tatizo na nakushukuru sana unapotuandikia, tatizo hatusomi. Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliwashinda wenzake wote kwenye mikutano *because he was a very good reader*, anasoma haraka haraka wakienda kwenye kikao kila kitu anakijua yeze, mwisho watu wote wanabaki wanapiga makofi tu, hata kwenye chama wanakaa kubadilisha jina wanasema hamjasoma hapa inasema nini.

Hoja ya Utanganyika watu tumekazana hapa kaka zangu akina Mheshimiwa Njelu Kasaka, amewaacha waende mpaka dakika ya mwisho akasema anataka kukutana na Wabunge. Hiyo hoja inatoka wapi, anaanza kusoma Sera ya Chama chetu inasemaje? Aaa, basi watu wamekwisha. (*Kicheko/Makofi*)

If you don't read you have no argument na ndiyo maana tunakupongeza sana Mheshimiwa Spika unapoandika hivi vitabu unagawa, lakini watu hawajafunua vile vitabu. Unatoa hizi *document* hapa watu hawaoni umuhimu wanaviacha vitu hivi. Vitu hivi ni muhimu sana, *people are not reading*, sisi tunathibitisha hapa. Sasa ninasema majukumu haya ni mazito. Ndicho chombo kikuu, lazima kiwe safi, lazima kiwe Kitakatifu.

Mheshimiwa Spika, la nne, kwa nini mama Saada Kitine anatajwatajwa na kwa nini hakuitwa ili ahojiwe. Kwanza hapo ndiyo ubinadamu wetu ulipoonekana kwamba huyu mama tunataku kumsumbu bure, pengine hata mambo hayo haelewi yanavyokwenda wa nini kumleta mama wa watu hapa, kwa nini kumsumbu, halafu mnamléta mbele ya mume wake wala siyo heshima hata kidogo. (*Kicheko/Makofi*)

Waliocheza ngoma hii ni wengine tu, pengine maskini alikuwa amejikalia pemberi sasa mama wa watu analetwa afanye nini. Kwanza mama huyu amekuwa *very sincere*, alisema; "mimi ninachoomba nisipelekwe Mahakamani," anayo barua aliyomwandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, alimwandikia Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, mimi ninaomba nisipelekwe Mahakamani, alitoa ombi hilo, lakini deni nitaendelea kulipa. Watu wanakutana wanasema hapana, licha ya ombi la kutopelekwa Mahakamani, wewe kwanza unashamehewa zote. Hoja hiyo yote inaondolewa, halafu hilo deni umesamehewa. Halafu shilingi 15,000,000/= Serikali ikurudishie.

Mheshimiwa Spika, asubuhi yake tulisoma katika Magazeti taarifa zimeandikwa; “Mama Kitine asafishwa,” “Wabunge Wote na Mawaziri Wameoza” na kadha wa kadha si imeandikwa kwenye magazeti na mmesoma leo asubuhi kwenye taarifa. Sasa kama ni huruma tu, lazima ziwe na kiwango.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa watoto wangu ni mkali na kila anayekuja anasema kweli umelea watoto. Nimewaambia sina *gold* wala *silver*, ni mimi na Mbunge ni Eliachim Simpasa tu, siyo ninyi. Kama kuna anayetaka Ubunge atagombea yeche mwenyewe. Nimewapa hela kila mmoja afanye shughuli zake, hakuna kuja nyumbani kwangu, mje mnisalimie tu lakini kuntegemea hakuna. Niliobaki nao nyumbani ni watoto wadogo wa *Form Four*, darasa la nne, darasa la pili tu, wengine waliosalia *out*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwa na lele mama, haiwezekani. Suala hili ni zito. Mnatakiwa ninyi muishauri Serikali, muihoji. Wakati ninyi wenyewe mnafanya *forgery*, mnafanya uongo, sasa unamwandama Waziri wa nini wakati wewe mwenyewe unafanya hayo?

Mheshimiwa Spika, kumetolewa hoja kwamba tunawaadhibu wananchi kwa kosa la Wabunge wao kukaa nje ya Bunge. Wala hakuna adhabu yoyote. Kuna Wabunge wengine kwenye Jimbo hata kutembelea hawatembelei. Wako Wabunge humu Mheshimiwa Rais amekwenda kwenye Majimbo yao, wakamwambia Rais, mzee ndiyo tunamwona leo hapa.

Kwa hiyo, wala wananchi hawatetereki kwa sababu mtu fulani haendi ni kisingizio tu, wananchi wana shughuli zao wewe usipokwenda wanaendelea kama kawaida na mara nyingi ukienda wanapata taabu, watafute kuku, watafute mbuzi na nini. Hamna lolote kuhusu hoja ya namna hiyo. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, katika wale waliosimama, hakuna ambaye alipendekeza tofauti kwamba adhabu isitolewe. Lakini katika wale walioniandikia, kuna mmoja aliandika wapewe onyo kali, onyo kali, la nini? Mwingine akasema wasipewe adhabu yoyote, *you are not serious* na kweli lama Bunge lako lingekataa adhabu leo hapa, ningejiu zulu. Kazi hii ni ngumu. Kazi ya kushughulikia masuala ya nidhamu ni ngumu na ni *very dangerous in life*, nimejitoa.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaipongeza Kamati yangu, ninao watu wenyewe busara. Safari hi wakati wanachagua Mwenyekiti sikuwepo nilikuwa Zambia, ila wakasema tunafikiri Mheshimiwa Eliachim Simpasa aendelee. Niliporudi kutoka Zambia wewe ukaniita, ukasema wenzako wamekuchagua tena, nilifikiri nimekwepa kwa kwenda Zambia, kumbe sijakwepa bado.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba nimejitoa mhanga kabisa, ni *very dangerous*, halafu watu wanaona kama ni kitu cha kawaida. Watu wanafanya *forgery*! Ninaomba tufike mahali wazee wenzangu Bunge liheshimike. Lazima watu wawe na imani na Bunge. Wakiona mtu ambaye ni mla rushwa au mtu wa ovyo kule waseme tunakwenda kumwambia Mbunge, tutakwenda kumwambia Mbunge. Lakini hali ikifika Mbunge mwenyewe....

MBUNGE FULANI: Anakula rushwa.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNG: Mbunge mwenyewe ndiye mla rushwa, haiwezekani wakaja tena.

Mheshimiwa Spika, sisi ambaa ni Walimu, tulipokuwa kule vijijini, watu wakianza kubishana, maana wakati ule kazi ya Ualimu ilionekana ni kazi Takatifu, kazi ya wito, wanasema ngoja tukamwulize Mwalimu, hawasemi tukamwulize Mganga wala sijui mtu fulani hapana. Wasomi wako kijijini, lakini wa kwenda kuulizwa ni Mwalimu, wakati huo Ualimu ulikuwa ni Ualimu kweli siyo Ualimu ambaa sasa hivi tunakwenda nao. Ulikuwa ni Ualimu hasa, unawajibika, watoto wote wa kike na wa kiume ni watoto wako, *seriously* ni watoto wako. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tumefikia hapa tulipo, ninaomba sasa nihitimishe hoja yangu. Kwanza ninashukuru sana kwa nafasi uliyotupa lakini vile vile ninashukuru kwa wale waliochangia. Sasa ninataka kutoa hoja kwamba kwa niaba ya Kamati yangu, ninaomba kupendekeza kwamba Waheshimiwa Wabunge wote waliotajwa, amba ni Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mheshimiwa Richard Ndassa, pamoja na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, wapewe adhabu ya kutohudhuria Mkutano huu wa Bunge la Bajeti kuanzia leo tarehe 10 Juni, 2003 hadi tarehe 7 Agosti, 2003 na Mtumishi wa Ofisi ya Bunge, Ndugu Elisa Mbise, suala lake lipelekwe kwenye Tume ya Huduma za Bunge kwa maamuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Hoja ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu
Kusimamishwa Kazi ya Ubunge Kuanzia Tarehe 10 Juni, 2003
Mpaka 7 Agosti, 2003 Ilipitishwa na Bunge*)

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge waliotajwa hapo juu waliondoka katika Ukumbi wa Bunge Kama
Walivyoamriwa*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kazi zilizopangwa kwa siku ya leo zimefikia mwisho. Kwa hiyo sasa kwa mujibu wa Kanuni zetu, ninaahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Hoja ya ...

SPIKA: Unasema hoja ya nini sijasikia *Chief Whip* unasema nini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Samahani, hoja ya kuahirisha Bunge.

SPIKA: Unafikiria kizamani, siku hizi Spika amepewa uwezo wa kuahirisha Bunge. Kwa hiyo, Bunge limeshaahirishwa mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Kicheko/Makofii*)

(*Saa 11.40 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano
Tarehe 11 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi*)

